**MSAKO** wamiliki silaha kinyemela rasmi Novemba

UKURASA 3



**TCU** yaongeza siku sita udahili kwa vyuo vikuu

UKURASA 5

**VILIO** vyatawala Kifungo maisha kwa kusafirisha dawa za kulevya

UKURASA 5




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Oktoba 5, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581820

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US





# Rais Samia afichua mianya ukwepaji wa kodi

**ATAKA** tume ichunguze, wafanyabiashara walia kero EFD... *Endelea ukurasa wa 2*

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan akizungumza kabla ya kuzindua Tume ya Rais ya Maboresho ya Kodi, Ikulu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# WARIOBA ASISITIZA MARIDHIANO KABLA UCHAGUZI

UKURASA 3



Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Sinde Warioba, akifafanua jambo wakati wa mahojiano na waandishi wa habari, Oysterbay Dar es Salaam jana. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

## RIPOTI MAALUM

## Simulizi ya aliyenusurika kifo TB sugu

UKURASA 4

**MICHEZO** **GAMONDI: MIPIRA YA FAULO 'KUWAUA'** UK 24

**MAONI, KATUNI UK.6**

# ...Wafanyabiashara walia kero EFD

**Na Maulid Mmbaga**

WAFANYABIASHARA na wadau wa masuala ya kodi, wamelalamikia mfumo wa matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) kuwa na mlolongo mrefu na kugeuka kero.

Kutokana na hali hiyo, wameiomba serikali kubuni njia za kisasa za kukusanya kodi.

Wamesema mfumo huo kwa upande wa halmashauri unaleta matokeo chanya lakini kwa wafanyabiashara wa chini wanaona kama umeletwa kuua biashara badala ya kuziendeleza.

Wafanyabiashara waliyasema hayo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa kongamano la kodi, lililoandaliwa na kampuni ya ushairi wa masuala ya kodi ya Oasis.

Mfanyabiashara katika soko la kimataifa la Kariakoo, Renatus Mlelwa, katika maoni yake, alisema changamoto hiyo ndiyo husababisha migomo ya wafanyabiashara Tanzania kuwa mingi.

"Mfumo huu si kwamba umekuja kuchangamsha biashara, unaweza kusaidia kukusanya mapato, lakini si kwa kiwango kikubwa.

"Ninapendekeza tuangalia nchi zingine operesheni hizi za kamatakamata hazipo, lakini kodi wanakusanya kwa kiwango kikubwa.

"Tuna haja ya kuja na mfumo mzuri wa kodi ambao watu wanalipa kodi nyingi, lakini pasipo na usumbufu au hizi kamatamamata kwa kuwa wafanyabiashara wadogo tumeona ni kilio na zinafukuza sana wageni.

"Mtu ametoka amenunua mzigo unamuuliza risiti, hivyo pamoja na utafiti unaofanywa hiki kitengo cha EFD kiangaliwe sana," alishauri Mlelwa.

Mlelwa alisema sera za kodi ambazo zinatumika sasa ni za zamani na kushauri mamlaka kuja na mawazo mapya, akitolea mfano China ambayo ilishatoka katika hatua hizo na kwamba ili kutoza lazima waangalie mtu aliuza kiasi gani.

"Tuje na njia za kisasa za kukusanya ambazo serikali itapata lakini wafanyabiashara watafanya biashara kwa uhuru na kwa amani.

"Wafanyabiashara tuko tayari kulipa, lakini tuleteeni mfumo rahisi wa kodi, kanuni za kipindi hicho tuachane nazo, tuje na mawazo mapya, sisi tumeng'ang'ania EFD wanatucheka sana, hivyo suala hili ni changamoto kubwa kwetu sio kwamba hatuitaki kulipa, tunataka ila tatizo ni mfumo," alisema Mlelwa.

Mfanyabiashara mwingine sokoni hapo, Justine Massawe, alisema mashine ikiharibika kama yuko mwenyewe dukani hulazimika kufunga duka kwenda Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ili kupewa kibali ili wakala aitengeneze.

Alisema Kariakoo kuna wafanyabiashara huanza biashara kwa mtaji kati ya Sh. 600,000 hadi Sh. milioni moja lakini mashine ya EFD anayotakiwa kuwa nayo inauzwa Sh. 500,000.

Mkrugenzi Mtendaji wa Oasis, Stambuli Myovela, alisema EFD ndio mzizi mkubwa wa matatizo ya Kariakoo.

Alisema wafanyabiashara na TRA kila mtu ana wajibu wake na kuna vitu ambavyo serikali inaendelea kuvirekebisha.

Myovela alisema shida kubwa ya EFD ni pale wafanyabiashara wanapoingiza mizigo kutoka nje ambayo ilisafirishwa kwa pamoja, lakini mmiliki kuwa zaidi ya mtu mmoja.

Mkurugenzi wa Elimu kwa Mlipakodi na Mawasiliano wa TRA, Richard Kayombo, alisema mlolongo wa taarifa ambazo mfanyabiashara anatakiwa kuziingiza kwenye mfumo wa EFD, ikiwamo namba ya utambulisho wa biashara (TIN), anuani, jina na sehemu anakofanyia kazi, ni za kawaida na hazina ugumu wowote.

Kayombo alisema taarifa hizo ni muhimu kwa mfanyabiashara na haziepukiki na hata akienda taasisi zingine zikiwamo za kifedha zitahitajika.

Alisema nyaraka hizo husaidia kulinda biashara na kutoa wito kwa Watanzania kwa ujumla kuwa wazalendo.

Kayombo alifafanua kuwa mashine EFD ikiharibika, mhusika anatakiwa kutoa taarifa TRA na ataipeleka kwa wakala aliyemuuzia kwa ajili ya matengenezo huku akipewa saa 48 ya kutumia risiti za mkono ambazo atatakiwa kuziingiza kwenye mfumo baada ya EFD kupona.

"Kuhusu suala la gharama, mfumo umeboreshwa na mtu anaweza kutumia simu janja kuweka programu husika ambayo ataitumia kutoa risiti, gharama ya mfumo huo ni Sh. 160,000, tofauti na mashine ambazo atanunua kwa Sh. 580,000," alisema Kayombo.

Kamishna wa Idara ya Walipakodi Wakubwa TRA, Michael Muhoja, alisema wanachotaka ni kuwe na uwanja sawa wa kila mmoja kufanya shughuli zake bila yeyote kuhisi kwamba hatendewi haki au anaonewa.

"Kama ni watu ambao tunalitakia mema taifa hili, tufuate sheria na utaratibu uliopo. Tukifanya biashara kila mtu kivyake hiyo ndiyo changamoto," alisema.



Msimamizi wa Miradi ya Wakala wa Nishati Vijijini (REA) Kanda ya Kati, Mhandisi Aneth Malingumu, akitoa taarifa kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, Adam Malima (kushoto), kuhusu upatikanaji wa umeme katika vijiji vya mkoa huo, wakati wa hafla ya kumtambulisha mkandarasi aliyeshinda zabuni ya kutekeleza mradi wa kupeleka umeme katika vitongoji mkoani humo, jana. Wa pili kushoto ni Katibu Tawala wa Mkoa huo, Dk. Mussa Ali Mussa. **PICHA: REA**

# Rais Samia afichua mianya ukwepaji kodi

**Na Beatrice Shayo**

RAIS Samia Suluhu Hassan amesema mrejesho alioupata katika ukusanyaji wa kodi ni kuwapo kwa malalamiko ya mianya ya ukwepaji wa kodi, makusanyo kidogo, huku mengi yakiingia mifukoni mwa watu.

Pia amesema baadhi ya watumishi wa serikali si waadilifu na kuna utaratibu usioridhisha katika utoaji wa misamaha ya kodi kwa wawekezaji.

Rais Samia aliyasema hayo jana Ikulu, Dar es Salaam, wakati akizindua Tume ya Rais ya Kutathmini na Kushauri Masuala ya Kodi.

"Hapa kuna malalamiko makubwa sana. Ni dhahiri kuna idadi kubwa ya sekta isiyo rasmi ambayo inakadiriwa zaidi ya asilimia 60 ya uchumi na hali hiyo inachangiwa na mfumo wa kodi kutovutia urasimishaji wa biashara na kutozingatia uleaji wa biashara zinazoanza. Hapa napo kuna tatizo," alisema.

Rais alisema serikali inalenga kujenga uchumi jumuishi unaokua kwa kasi na kuimarisha ustawi wa watu kwa kuboresha huduma za jamii na kupunguza umaskini wa kipato kwa mtu mmoja mmoja.

Alisema mambo yanayotakiwa kufanywa ili kufikia hatua hiyo, kwanza ni amani na utulivu katika nchi ambapo Tanzania jambo hilo liko vizuri.

"Tunajaribu kuhakikisha nchi yetu inabaki na amani na utulivu na wakuu wa vyombo wapo hapa na tunawashukuru mmefanya hiyo kazi," alisema.

Jambo la pili, Rais Samia alisema ni suala la mifumo ya haki inayoeleweka hali iliyosababisha kuunda tume ya kuangalia haki jinai ambayo ilifanya tathmini nchi nzima na kutoa mapendekezo.

"Kwa kiasi kikubwa mahakama wametekeleza vizuri, wako asilimia 70 ya utekelezaji lakini vyombo vingine navyo Jeshi la Polisi, DPP (Mwendesha Mashtaka Mkuu wa Serikali) na kwingine nako wanaendelea kutekeleza," alisema.

Alitaja jambo la tatu ambalo linaifanya nchi itoke hatua moja kwenda nyingine ni mifumo mizuri ya kodi ili ilipwe kwa urahisi na kwa wakati bila misuguano.

"Wafanyakazi kila siku utasikia tupunguzie kodi kubwa na wafanyabiashara na wao malalamiko. Jambo la kodi halijawahi kuwa rahisi kutokana na ushirikiano na wadau mbalimbali. Serikali imeamua kulifanyia kazi suala la kodi nchini pamoja na mambo mengine," alisema.

Rais Samia alisema wameimarisha mifumo ya ukusanyaji mapato na kuijengea uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara nchini na kuchangia kuleta matokeo chanya ambapo makusanyo ya kikodi yameongezeka kutoka wastani wa Sh. bilioni 850 kwa mwezi mwaka 2015 hadi wastani wa Sh. trilioni mbili kwa mwezi mwaka 2023.

Alisema takwimu za makusanyo ya mwezi uliopita zinaonesha walikusanya zaidi ya Sh. trilioni tatu.

"Eneo hilo ni muhimu kusimamiwa vizuri ili kuongeza ukuaji wa uchumi wa nchi. Uchumi unakua ila hauakisi uhalisia wa kile kinachokusanywa. Kinachokusanywa ni kidogo kingi kinaingia mifukoni mwa watu bure.

"Shughuli za kiuchumi zinazoendelea nchini na idadi ya watu haiakisi uhalisia kukua kwa uchumi na shughuli mbalimbali za kiuchumi na idadi ya watu haiendani na mapato tunayoyapata," alisema.

Alisema vyanzo vya ndani na visivyo vya ndani vya kodi vipo chini ya lengo walilojiwekea.

"Miongoni mwa viashiria vya utulivu wa uchumi jumla vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano hadi mwaka 2026 ni kuongezeka kwa pato la kodi hadi kufikia asilimia 14.4. Kiwango hicho kitawawezesha kujitegemea.

"Kwa mujibu wa TRA, mwaka 2023/24 mapato ya kodi yamefikia asilimia 12 ya pato la taifa, hivyo bado wapo chini, kuna kazi ya kufanya," alisema.

Alisema mifumo ya kielektroniki kwa taasisi za serikali zinazotoa leseni kutokusomana ni jambo jingine ambalo linalalamikiwa.

"Kutokuzingatia weledi wakati wa ukusanyaji wa kodi mfano matumizi ya nguvu, lugha zisizo na staha na ubabe kwa baadhi ya watumishi wa serikali hayo nayo yanalalamikiwa.

"Nilikuwa Ruvuma mama lishe analalamikia mikopo ya asilimia 10 ya halmashauari anaenda kufanya biashara ya Sh. 10,000 TRA wanakusubiri, nikasema TRA kwa mama lishe anafanya nini, haya nayo ya kwenda kuyatizama," alisema.

Alisema idadi ya walipa kodi ni wachache ni zaidi ya milioni mbili kati ya watu milioni 66 wakitoa watoto na watu wengine ambao hawastahili kulipa kodi, hawapungui milioni 37 wanaoweza kulipa kodi.

Rais Samia alisema ameunda tume hiyo ili iwasaidie kufanya tathmini ya mfumo mzima wa kodi kwa upana wake lengo ni kuimarisha zaidi mazingira ya biashara na uwekezaji, kurahisisha usimamizi wa ukusanyaji wa kodi nchini.

Alisema ili isaidie kutathmini, kuchambua na kutoa mapendekezo ya kuimarisha mfumo mzima wa kodi kuendana na mabadiliko ya kiuchumi na kijamii ikiwamo matumizi ya teknolojia.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Makulu ya jijini Dodoma, wakipata mafunzo ya umuhimu wa kuweka akiba ya fedha kutoka kwa Mkuu wa Kitengo cha Kiatamizi cha Biashara Benki ya Stanbic Tanzania, Kai Mollel, kupitia programu ya Elimu ya Fedha, shuleni hapo, mapema wiki hii, ikiwa ni sehemu ya mikakati ya kuboresha elimu katika jamii, kwenye safari ya Baiskeli ya Twende Butiama 2024. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Warioba asisitiza maridhiano kabla uchaguzi

**Na Christina Mwakangale**

WAZIRI Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, amesema kuna haja ya kuwapo maridhiano na kuondoa kasoro zilizojitokeza mwaka 2019 na 2020 wakati wa kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Amesema uchaguzi wa vipindi hivyo tofauti, ulikuwa na dosari ambazo baadhi ni ngumu kuepukika, ingawa kadiri kasoro zinapobainika, kuna haja ya kufanyiwa kazi ili kujenga imani kwa pande zote, wananchi na vyama vya siasa.

Jaji Warioba aliyasema hayo jana Dar es Salaam, alipozungumza na waandishi wa habari, kuhusu masuala mbalimbali ya nchi yakiwamo siasa na uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika mwezi ujao. Alionya kuwa kasoro kuu ya rushwa miongoni mwa wagombea isipofanyiwa kazi inaweza kusababisha matatizo.

"Ni kweli kwamba kila uchaguzi una dosari. Duniani nako hakuna ambako hakuna dosari. Ziko za kawaida, ndogo ndogo na uchaguzi unaofuata unakuwa mzuri zaidi. Lazima tukubali katika uchaguzi unaokuja, tumelizungumza sana kwa sababu ya matukio yaliyotokea mwa 2019 na 2020.

"Katika maisha yangu nimeshapiga kura kwa takribani miaka 13 tangu tupate uhuru na kila baada ya miaka mitano lazima tuwe na uchaguzi. Kwa kipindi chote hiki hakukuwa na matatizo makubwa katika uchaguzi, ukiacha yaliyotokea Zanzibar," alisema.

Alisema uchaguzi wa serikali za mitaa kwa mwaka 2019 na uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 ulikuwa na kasoro kubwa na kusababisha baadhi ya watetezi wa haki za binadamu na demokrasia, kushtuka na kuwa miongoni mwa hoja kuu kuwako kwa uhuru na haki kwa uchaguzi ujao.

"Mfano mwaka 2019 tunapozungumzia dosari kipindi hiki kulikuwa na dosari nchi nzima hasa katika uteuzi wa wagombea, usimamizi wa uchaguzi na wajibu wa mawakala. Mwaka huu kuna jitihada kubwa za kufanya ili yaliyotokea yalisitokee tena.

"Serikali za mitaa tumefanya kwa miaka mingi na hata tulipoingia mfumo wa vyama vingi, ulisimamiwa na serikali mwaka 1994 mpaka 2014 hakukuwa na matatizo makubwa.

Ule wa mwaka 2019 ulikuwa kama umepangwa matatizo haukuwa wa kawaida. Mwaka huu pia uchaguzi wa serikali za mitaa utasimamiwa na serikali, maandalizi yamefanyika. Elimu ni muhimu kwa sababu bila hilo inawezekana uchaguzi wa mwaka huu usiwe na matokeo makubwa," alisema.

Jaji Warioba alisema uchaguzi ulio huru na wenye haki utaziondoa kasoro zilizotokea awali kwa kuwapo hakikisho hasa wakati wa kuteua wagombea hakutakuwa na tatizo, kwa baadhi yao kuenguliwa.

Pia alisema maandalizi wakati yanakwenda vyema hivi sasa kama vile ya kujiandikisha, kuwako elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kupiga kura kwa sababu uzoefu unaonesha idadi ya wapigakura nchini inapungua licha ya wengi wao kujitokeza katika kusikiliza sera za wagombea wanapojinadi kwenye kampeni.

"Yule aliyesimamia uchaguzi ndiye yule yule atasimamia. Bado wananchi wana wasiwasi, atarudia ile au atafanya tofauti? Kuna haja ya jitihada kuwaaminisha wananchi yaliyotokea nyuma hayatajirudia tena," alisema.

Warioba alisema kasoro zingine ni kuwa maandalizi ya kuwafanya wananchi wawachague wanaowataka ni duni, licha ya kwamba wapigakura wa kitongoji ndio wanaowafahamu wanaoishi eneo lao.

"Vyama vinapeleka watu wao (wateuliwa). Wakati wa mfumo wa chama kimoja, kulikuwa na utaratibu wa kujua, je, hawa wanakubalika? Kulikuwa na mkutano mkuu kwa ajili ya kupata kura za maoni, lakini nikaja na hoja mkutano mzima unaweza kuhongwa, tuite wote balozi hadi wenyeviti wa wilaya waje.

Lakini haikupita muda kumbe hata kundi hili kubwa kuna watu wana fedha nyingi wanaweza kuwahonga, tuite wanachama wote bado ikashindikana. Tatizo la rushwa likawa linaingilia uchaguzi, tukasema tuwe na wajumbe wa kupiga kura za maoni, bado tatizo," alisema.

Alisema wagombea wengi nchi nzima, wana uwezo wa kuwahonga wanaowapigia kura za maoni na kwamba ugumu unakuja kutokana na wanaohongwa ni viongozi watarajiwa kupigakura.

"Kwa hiyo hatuna uhakika tuliposema wananchi wana haki ya kumpata yule wanayemwona anafaa. Katika maandalizi, vyama vya siasa viwe na utaratibu ambao unazingatia wanaoteuliwa wanakubalika kwenye maeneo yao, kwa sababu wakichaguliwa wasiofaa hawatasaidia.

"Kwa sababu akiwa mteuliwa na chama lakini hakubaliki, inawapunguzia uwezo hawa viongozi. Kwa kuwa wananchi hawamkubali, inakuwa ngumu kuwaongoza, hivyo tunataka watu wanaokubalika na jamii," alisema.

Jaji Warioba alisema uongozi wa serikali za mitaa ni muhimu kutokana na kwamba ndiko unakoanzia uongozi na kubainisha kwamba uongozi wa ngazi ya chini kutokuwa thabiti imekuwa sababu ya jamii linapotokea tatizo, huitazama nafasi ya juu kiuongozi wakimtaka rais awatatulie matatizo yao.

Pia alisema kuna haja ya serikali, mamlaka za usimamizi wa uchaguzi kukaa meza moja na vyama vya siasa kuvihakikishia amani, akionya kuwa matumizi ya nguvu ya vyombo vya ulinzi na usalama, tija yake hupungua kutokana na pande zote kushindana.

Jaji Warioba alisema kwa kipindi cha takribani miongo mitatu demokrasia imejengwa, ingawa utawala bora uliwekwa nyuma na kwamba ni wakati wa kuujenga, kwa kuwa ndio msingi wa uongozi.

"Miaka mitatu iliyopita hali ya siasa haikuwa nzuri. Maandamano yalizuiwa, mikutano ilipigwa marufuku. Rais (Samia Suluhu Hassan) ameiweza nchi sasa imetulia kwa sababu aliondoa yale matatizo. Mfano haya maandamano ya hivi karibuni mimi ninachokiona ni kupambana.

"Jeshi la Polisi linasema watakaokuja watakiona na vyama vya siasa nao wanakuja na wanachokitaka. Watumie lugha nzuri katika shughuli za siasa zetu. Amani inajengwa na wananchi na si polisi peke yao, maana wanasema wanalinda amani, mi nadhani wakae chini pande zote, wakubaliane," alisema.

# Msako wamiliki wa silaha kinyume cha sheria kuanza rasmi Novemba

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi nchini limesisitiza baada ya mwezi huu kuisha msamaha uliotolewa kwa wamiliki wa silaha kinyume cha sheria kuzisalimisha, linatarajia kuanza msako dhidi ya waliokaidi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, Naibu Kamishna wa Polisi (DCP), David Misime, aliyasema hayo jana na kusisitiza watakabainika bado wanatumia silaha hizo kinyume cha sheria, hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yao.

Misime alisema lengo la kutangaza msamaha huo ni kuhakikisha silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria zinaondoshwa katika jamii ili zisisababishe madhara kwa raia yakiwamo vifo, majeruhi, watu kuhama makazi, njaa pamoja na uchumi kuzorota.

Alisema masharti yaliyotolewa katika tangazo hilo la msamaha ni pamoja na kipindi cha usalimishaji wa silaha zinazomilikiwa kinyume cha sheria kilichoanzia Septemba Mosi hadi Oktoba 31, mwaka huu.

"Maeneo ya usalimishaji wa silaha hizo ni vituo vya Polisi, Ofisi za Serikali za Mitaa na katika Ofisi za Watendaji Kata/Shehia pamoja na muda wa usalimishaji wa silaha ambao ni kuanzia saa mbili asubuhi hadi saa kumi jioni," alisema.

Misime alizitaja silaha zinazopaswa kusalimishwa ni pamoja na zile ambazo hazijawahi kusajiliwa nchini na zimekuwa zikimilikiwa kinyume cha sheria na zile awali zilikuwa zinamilikiwa kihalali, lakini kwa sasa wamiliki wamefariki dunia na ndugu kuendelea kuzimiliki kinyume cha sheria.

"Jeshi la Polisi linawahakikishia wananchi kuwa yeyote atakayesalimisha silaha hizo ndani ya kipindi cha msamaha hatoshtakiwa na wala hakutohitajika kujua jina la atayesalimisha au kujua uhalifu uliotendeka kwa kutumia silaha hiyo," alisema.

Takwimu zinaonesha mwaka 2023, silaha 337 na risasi 262 zilisalimishwa kwa hiari na baada ya msako ulifanyika nchi nzima na watuhumiwa 176 walikamatwa na silaha 195.

Pia walikamatwa watuhumiwa saba ambapo wanaume walikuwa sita na mwanamke mmoja ambao walikutwa wakimiliki risasi 334 kinyume cha sheria na kufikishwa mahakamani na baadhi walitiwa hatiani na kutumikia kifungo gerezani na wengine kesi zao zipo katika hatua mbalimbali.

# Simulizi aliyenusurika kifo kwa TB sugu

**Na Romana Mallya**

"NILIKUWA marehemu mtarajiwa. Nilipotolewa mgodi wa Tanzanite Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, kupelekwa hospitalini. Nyumbani walikuwa wameanza maandalizi ya mazishi yangu."

Hiyo ni kauli ya Labowa Ingwagwi (50), aliyekuwa kibarua katika mgodi huo kwa miaka mitano, akisimulia alivyougua kifua kikuu (TB) sugu mara mbili na kukatisha ndoto yake ya kumiliki fedha nyingi na kuishi nje ya nchi.

Akiwa na miaka 21 wakati huo, umri unaotajwa ni wa vijana wengi hadi sasa wa kukimbilia migodini au machimbo, Ingwagwi anasema kilichomsukuma kwenda huko kusaka dhahabu ni ugumu wa maisha mtaani.

Safari katika machimbo hayo aliianza mwaka 1995 akiwa mwenye ndoto zinazofanana na wenzake za kupata mawe ili kumiliki fedha nyingi.

"Nilikwenda Mirerani kwa sababu ya ugumu wa maisha kijijini wakati huo. Vijana wengi fursa ambayo tulikuwa tunaiona kwa haraka ni migodini au machimbo ya madini ambako baadhi waliorejea mtaani walionekana maisha yao yamebadilika.

"Nami nilivutiwa nikaona hakuna njia nyingine ya kupata fedha nyingi kwa haraka kama sitajiunga na vijana wenzangu kusaka mawe.

"Ukiwa huko hakuna kukata tamaa. Ndoto ni siku moja umiliki fedha nyingi. Nilitamani nikishapata jiwe nikaishi Afrika Kusini," anasimulia Ingwagwi ambaye amezaliwa katika Kijiji cha Riroda, Babati mkoani Manyara.

Kuhusu maisha yake Mirerani, anasimulia kuwa miaka ya mwanzoni ni ya kufanya kazi kwa bidii bila malipo.

"Kipindi hicho Mirerani kama unafanya kazi unahudumiwa chakula na mtu yeyote. Ilikuwa ule ukafanye kazi. Malipo ni mpaka upate jiwe. Nilifanya kazi ya bure kwa miaka karibu mitatu. Kule kuna hatua ya kufanya kazi za bure na hatua ya kutafuta riziki," anasema.

**NDOTO KUZIMIKA**

Anasimulia kuwa wakati amefikia hatua ya kuingia katika maeneo yenye matumaini ya kupata mawe, ndoto ilizimika ghafla na kuanza kuugua, mwili kudhoofu siku hadi siku.

Mwaka 1999, hali kiafya ikawa mbaya zaidi ndipo wenzake walipompeleka Hospitali ya Kibong'oto (Hospitali ya Rufani ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi ya Kibong'oto), iliyoko Siha mkoani Kilimanjaro (KIDH) na kugundulika ana TB sugu.



Labowa Ingwagwi (50), mwenyeji wa Kata ya Riroda, Kijiji cha Riroda, Wilaya ya Babati Vijijini, mkoani Manyara, akizungumza katika mahojiano maalum. **PICHA: ROMANA MALLYA**

"Nilipopata nafuu nilisimuliwa kuwa nyumbani kwetu waliponiona hospitalini walianza maandalizi ya mazishi yangu. Nilikaa miezi miwili hospitalini mpaka nilipomaliza sindano 60 na kuruhusiwa kwangu kulitokana na uaminifu nilioonesha kwa wauguzi.

"Ili mgonjwa wa TB uruhusiwe kwenda nyumbani kuendelea na dozi ya vidonge, ni lazima kuonesha uaminifu katika umezaji dawa kwa wakati na muda uliopangwa, kinyume cha hapo hutoruhusiwa. Matibabu yangu yalichukua miezi sita," anasema.

**TB MIGODINI**

Ingwagwi ambaye ni mtoto wa tano kati ya wanane, wakiwa idadi sawa kijinsia, anasema baada ya kutibiwa, wataalamu wa afya walimweleza sababu ya kupata TB sugu ni shughuli za migodini, hivyo akashauriwa kutorejea huko na kutojihusisha na shughuli ngumu kulingana na hali yake ya afya baada ya matibabu.

Anasema daktari wake alimweleza kuwa chanzo cha maambukizi ya TB migodini ni zile kazi zinazohusisha kuzama ardhini wakati mwamba umelipuliwa na kabla vumbi halijatulia wao tayari wameshaingia. Pia uvutaji wa ulanga wa madini ambao kuingia kifuani na kubaki.

"Migodini tunashirikiana mambo mengi na wakati mwingine tunalala 'geto' (chumba) kimoja vijana wanne au zaidi, hivyo mtu akiwa na ugonjwa wa kuambukiza kama TB anatema makohozi popote ni rahisi kuambukizana," anasema.

**KUREJEA KIJIJINI**

Anasema baada ya ushauri huo, aliporuhusiwa hospitalini alirejea kijijini kwao Riroda na kwa kuwa hakuwa na kipato chochote maisha yakawa ya shida zaidi na kushindwa kujihusisha na shughuli ngumu kama mtaalamu wa afya alivyomshauri.

"Wakati huo sikuwa na mke wala mtoto. Nikarejea nyumbani kuanza upya. Yale maisha ya kupewa ugali na wenzako yakawa hayapo. Nilipitia hali ngumu, sikuweza kuepuka kufanya kazi ngumu. Mwezi Aprili, mwaka 2010, TB sugu ikanirudia na kuanza kutapika damu.

"Ilirudi kwa sababu nilikuwa ninabeba magunia yenye uzito mkubwa kupata fedha za kujikimu. Pia nilikuwa ninaingia katika ghala la nafaka ambako kuliwekwa dawa ambazo ni kisababishi pia," anasema.

Anasema alirudishwa hospitalini na kukaa siku 72 na alipomaliza sindano 60 aliendelea na dozi ya vidonge alivyotumia kwa miezi 12 akiwa nyumbani hadi alipopona.

**ATUNUKU TUZO HOSPITALI**

Ingwagwi mwenye watoto sita wa kwanza akiwa na miaka 20, anasimulia kwamba kuugua hadi kuchungulia kaburi, matibabu aliyopewa hadi kupona TB sugu, kumemfanya kuitunuku tuzo maalum Hospitali ya Kibong'oto.

"Kilichonisukuma ni wakati ninaendelea na matibabu wodini ya kupigania maisha, mwaka 2010 kwa mara ya kwanza nikiwa wodini, nilishuhudia sherehe ambayo baadaye niliambiwa ni Siku ya Wauguzi Duniani, inaliyofanyika mwezi Mei.

"Niliwaangalia madaktari na manesi walivyokuja kutufariji na ikanikumbusha hali ya mahututi niliyopitia. Wakatupa zawadi ya sukari, sabuni na shuka. Walifanya hivyo ni wauguzi waliokuwa wanatuhudumia.

"Wakati ninaruhusiwa nilimwambia daktari, ninakwenda nyumbani, nikamwomba wakati mwingine wakiandaa sherehe kama hiyo wanishirikishe," anasema.

Mwaka 2021, anasema alipokea simu kutoka kwa nesi hospitalini hapo akimjulisha kuhusu sherehe wanayotarajia kufanya. Anasema alipohudhuria walimpa heshima ya kuwa mgeni maalum na yeye kutumia fursa hiyo kutoa ushuhuda wake na kuahidi kuwapa zawadi maalum.

Ingwagwi anasema mwaka 2022, 2023 hawakufanya sherehe, hivyo Julai 4, mwaka huu, aliamua kuandaa tuzo maalum na kuwasiliana na Mkurugenzi wa Hospitali hiyo na kwenda kuikabidhi.

Anasema amefanya hivyo kwa sababu ametambua umuhimu wa wahudumu wa afya ambao wamekuwa wakifanya kazi usiku na mchana kuokoa maisha ya wagonjwa.

"Kwa hali niliyokuwa nayo wakati ninaugua nilikuwa tayari kwa lolote kufa au kupona. Niliwapenda sana walivyonihudumia. Si mimi peke yangu, hata wenzangu walihudumiwa vizuri. Nyumbani walikuwa wanaogopa kushika makohozi, damu na kuninyanyapaa.

"Lakini hospitalini nesi anakushika, anakusafisha ni kitendo ambacho nilisema sitasahau. Ndiyo maana nimetengeneza tuzo kwa kutambua mchango wao katika kuokoa Watanzania wanapougua," anasema.

Wakati Ingwagwi akisimulia madhila hayo, Anna Joseph, mkazi wa Kimara, Kinondoni, Dar es Salaam, anaeleza changamoto alizopitia katika kumuuguza mdogo wake wa kiume aliyefariki dunia kwa TB sugu mwaka 2021, baada ya kumuuguza zaidi ya miaka 10.

Anasema mdogo wake aliyekuwa akifanya kazi mgodi wa Mirerani, aligundulika rasmi kuwa na TB mwaka 2009, wakati huo akiwa na umri wa miaka 30 na alipotibiwa tofauti na Ingagwi, alirejea mgodini.

Ingwagwi anasema kuanzia mwaka 2013 mdogo wake aliugua kwa ugonjwa kujirudiarudia, hivyo kutumia dawa zaidi ya mara saba hadi alipofariki dunia.

"Wakati ninamuuguza nilichogundua ni anayeumwa anakuwa na hofu ya kupona kwa sababu anakuwa amekunywa dawa zaidi ya mara mbili. Wakati mwingine anakuwa kama hakuamini unayemuuguza, anaona kama unamkatia tamaa na kuna wakati anaona kama unamsanifu.

"Kwa upande wa gharama ni kubwa kuanzia matunzo. Wanatakiwa kutumia asali wa nyuki wadogo lita moja ni zaidi ya Sh. 20,000," anasema.

Anasema kumpeleka hospitalini inabidi kutumia usafiri binafsi kulingana na hali ya mgonjwa na kama familia haina uwezo ni changamoto.

"Wanachoka, mfano mdogo wangu ametumia dawa zaidi ya mara saba na alikuwa na magonjwa nyemelezi ambayo nayo kuyatibu ni gharama. Mfano anapata Nimonia (maambukizi kwenye mapafu) au fangasi kwenye mapafu, anahitaji CT-Scan kama huna fedha ni shida," anasema.

**Itaendelea kesho**



## HABARI KITAIFA




Katibu Mtendaji wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Prof. Charles Kihampa, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dodoma jana, kuhusu kufunguliwa awamu ya tatu ya dirisha la udahili wa Shahada ya Kwanza, unaoanza leo hadi Oktoba 9. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Vilio vyatawala hukumu maisha kusafirisha dawa za kulevya

**Na Kulwa Mzee**

VILIO vyatawala katika ukumbi wa wazi wa Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi baada ya mahakama hiyo kumtia hatiani mshtakiwa Saidi Mbasha na wenzake wawili na kuwahukumu kifungo cha maisha jela kwa kusafirisha dawa za kulevya.

Washtakiwa hao walitiwa hatiani jana mbele ya Jaji Sedikia Kisanya baada ya kupitia ushahidi wa upande wa mashtaka na utetezi wa washtakiwa wote wanne.

Hata hivyo, mahakama ilimwachia huru mshtakiwa wa nne, Fatuma Shomari, baada ya kujiridhisha kwamba hana hatia katika kosa alishtakiwa nalo. Mbali na Mbasha, washtakiwa wengine waliotiwa hatiani ni Joseph Dalidali na Allu Murungwa.

Akisoma hukumu hiyo, Jaji Kisanya alisema washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na mashtaka mawili. Shtaka la kwanza linawakabili washtakiwa wote na la pili likimkabili Mbasha na mkewe, Fatuma Shomari, walidaiwa kukutwa na bangi gramu 2.63.

Alisema katika shtaka la kwanza, Machi 3, 2021 maeneo ya Kinondoni, washtakiwa walikutwa na dawa za kulevya aina ya heroine kilo 29.89. Katika kuthibitisha mashtaka, upande wa Jamhuri uliita mashahidi tisa na upande wa utetezi washtakiwa walijitetea wenyewe.

Jaji Kisanya alisema baada ya pande zote mbili kufunga ushahidi, walifanya majumuisho ya kesi na mahakama katika kufika uamuzi ilizingatia hoja zilizomo kwenye majumuisho hayo.

"Mahakama imejiridhisha kwamba kielelezo ni dawa za kulevya, washtakiwa ndio walisafirisha, upekuzi na ukamataji ulifuata utaratibu wa kisheria na vielelezo vilitunzwa kwa usahihi.

"Upande wa mashtaka umethibitisha kwamba dawa zilizokamatwa ni heroine kilo 29.89, mshtakiwa wa pili aliyeanza kukamatwa, alieleza kuwa dawa zilihifadhiwa Kijitonyama.

"Mshtakiwa wa pili alimtaja mshtakiwa wa tatu kuwa mshiriki katika biashara hiyo ya dawa za kulevya na aliwaongoza Polisi hadi nyumbani kwa mshtakiwa wa tatu. Walipofanya upekuzi, walikuta mabegi mawili yakiwa na dawa za kulevya kilo 29.89," alisema Jaji.

Alisema mshtakiwa wa tatu alikubali kwamba mabegi mawili yalikutwa nyumbani kwake, yalipelekwa na mshtakiwa wa kwanza ambaye aliyachukua kutoka kwa mshtakiwa wa nne.

Jaji Kisanya alisema mshtakiwa wa kwanza, wa pili na tatu, walikuwa wakifahamu biashara hiyo na walikuwa wakifahamiana. Alisema mshtakiwa wa nne alikubali begi moja lilikuwa lake lakini haijulikani kama alikuwa anajua kilikuwa na nini ndani.

"Mshtakiwa wa kwanza alichukua begi bila kumjulisha anaenda kufanya nini. Kuna uwezekano alichukua begi bila mshtakiwa wa nne kujua, hivyo hakuhusika katika kosa," alisema.

Baada ya kupitia ushahidi, alisema upande wa Jamhuri umethibitisha kuwa mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa tatu walihusika kutenda kosa, hivyo mahakama inawatia hatiani kwa shtaka la kwanza na mshtakiwa wa nne anaachiwa huru kwa kosa lo pili aliloshtakiwa nalo pamoja na mshtakiwa wa kwanza baada ya kubainika kwamba shtaka halijathibitika.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Itike Mwaisaka, akisaidiana na Wakili wa Serikali Jesca Msae, waliomba washtakiwa wapewe adhabu kali. Pia waliomba dawa za kulevya ziharibiwe, Sh. milioni 12, Dola za Marekani 14,000 na gari moja, itolewe amri vitaifishwe kuwa mali ya serikali.

Mawakili wa utetezi, Constantine Kakula na Jeremiah Mtobesya waliomba mahakama impunguzie adhabu mteja wao, Allu, wakati wa tukio alikuwa mwanafunzi, hivyo hakujua hatari ya vitu hivyo.

Pia upande wa utetezi uliomba washtakiwa wengine wana tatizo la afya na wana familia zinawategemea, hivyo wapunguziwe adhabu.

Akitoa adhabu Jaji Kisanya alisema Sheria ya Dawa za Kulevya inasema ukipatikana na hatia jela maisha.

"Kwa shtaka la kwanza la kusafirisha dawa za kulevya, mahakama inawahukumu mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa tatu kutumikia kifungo cha maisha jela," alisema Jaji Kisanya na kumwachia huru mshtakiwa wa nne Fatuma.

Baada ya hukumu hiyo, vilio vilitawala ndani ya ukumbi wa mahakama kutoka kwa ndugu na jamaa waliofika kusikiliza hukumu hiyo. Mshtakiwa Allu aliangukia ndani ya kizimba baada ya kusikia adhabu ya maisha jela.

Mahakama imeamuru dawa za kulevya ziharibiwe na kuhusu kutaifisha Sh. milioni 12 na gari mahakama imewaelekeza upande huo kufuata masharti yaliyowekwa katika Sheria ya Dawa za Kulevya.

Jaji Kisanya alisema ikiwa hakuna hatua zitakazochukuliwa ndani ya muda, fedha hizo na gari zirudi kwa wahusika ambao ni mshtakiwa wa kwanza na mshtakiwa wa pili.

# TCU yaongeza siku 6 udahili vyuo vikuu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TUME ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) imetangaza awamu ya tatu na mwisho ya dirisha la udahili wa wanafunzi wa shahada ya kwanza vyuo vya elimu ya juu nchini utakaofanyika kwa siku sita.

Akizungumza na waandishi wa habari, Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema dirisha hilo lilifunguliwa kuanzia jana na litafungwa Oktoba 9, mwaka huu.

Prof. Kihampa alisema wanafunzi waliochaguliwa katika awamu ya pili ya udahili, wanatakiwa kujithibitisha katika vyuo walivyochaguliwa ifikapo Oktoba 21 mwaka huu.

Alisema baada ya kukamilika kwa awamu zote mbili, tume hiyo ilipokea maombi ya kuongeza muda kutoka kwa Jumuiya ya Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu (TAHILISO) kuwa wapewe muda wa kuendelea na kudahili.

"Kuna waombaji ambao hawakupata nafasi ya kudahiliwa au kutuma maombi katika awamu ya pili kutokana na sababu mbalimbali, sasa wanapaswa kutumia nafasi hii kutuma maombi katika vyuo hivyo. Hii ni nafasi ya mwisho," alisema Prof. Kihampa.

Alisema tayari TCU imeelekeza vyuo kutangaza programu ambazo bado zina nafasi na kuwataka waombaji kuzingatia utaratibu wa awamu ya tatu kama ulivyoainishwa.

Prof. Kihampa alisema waombaji waliodahiliwa katika chuo zaidi ya kimoja katika awamu ya pili na wale ambao hawakuweza kuthibitisha katika awamu ya kwanza, wanapaswa kuthibitisha udahili wao katika chuo kimoja kuanzia jana hadi Oktoba 21 mwaka huu.

"Uthibitisho huo ufanyike kwa kutumia namba maalum ya siri iliyotumwa kwa ujumbe mfupi kupitia namba za simu au barua pepe walizotumia katika udahili," alisema Prof. Kihampa.

Pia alisisitiza uthibitisho wa udahili ufanyike kupitia akaunti ambayo mwombaji aliitumia wakati wa kuomba udahili wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

Alisema kwa ambao hawatapata kwa wakati ujumbe huo, wanashauriwa kuingia katika mifumo ya udahili ya vyuo walivyodahiliwa ili kuuomba kumwezesha kuthibitisha katika chuo husika.

Prof. Kihampa alisema kwa wale ambao watapata changamoto katika kuthibitisha tayari vyuo vyote vimeelekezwa kupokea taarifa zao, ikiwamo kuzitafutia ufumbuzi wa haraka kwa kuzingatia miongozo na taratizu zote zilizowekwa.

Alisema vyuo vinatakiwa kuwasilisha TCU majina ya waliodahiliwa katika awamu ya tatu kuanzia Oktoba 13 hadi Oktoba 15, mwaka huu, na Oktoba 19 vyuo vinatakiwa kutangaza majina ya waliodahiliwa katika awamu ya tatu.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ufunguzi msimu mpya Ligi Kuu ya Wanawake wavutia

**FAINALI** ya Ngao ya Jamii kwa Wanawake kwa mwaka huu inatarajiwa kufanyika leo kwa kuwakutanisha 'Maafande' wa JKT Queens dhidi ya Yanga Princess, zote kutoka jijini Dar es Salaam.

JKT Queens ilifika hatua hiyo baada ya kuibamiza bila huruma Ceasiaa Queens kutoka Iringa mabao 7-0 wakati Yanga Princess ilipata ushindi wake wa kwanza wa penalti 4-3 dhidi ya watani zao, Simba Queens kutokana na kwenda sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90 za kawaida.

Mashindano hayo yanafanyika kwa mwaka wa pili baada ya mwaka jana yalipoanza, Simba Queens kufanikiwa kuibuka mabingwa.

Kuanza kwa mashindano hayo ni ishara ya ufunguzi wa msimu mpya wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania umekaribia, ligi hiyo inayotarajiwa kushirikisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali itaanza rasmi ifikapo Oktoba 9, mwaka huu.

Timu zinazotarajiwa kushiriki ligi hiyo ya juu ya wanawake nchini ni pamoja na mabingwa watetezi, Simba Queens, JKT Queens, Yanga Princess, Ceasia Queens, Fountain Gate Princess, Alliance Girls, Mashujaa Queens (zamani Amani Queens) na Bunda Queens ya Musoma mkoani Mara.

Gets Program ya Dodoma na mabingwa wa kwanza wa Ligi Kuu ya Wanawake kwa msimu wa 2016/2017, Mlandizi Queens kutoka Mlandizi mkoani Pwani pia zitashiriki ligi hiyo baada ya kupanda daraja.

Kufanyika kwa mashindano hayo ni kielelezo cha wazi kwamba mpira wa miguu wa wanawake Tanzania unaendelea kupiga hatua, michuano hiyo imeonekana kuvutia na timu zilizocheza mechi za hatua ya nusu fainali kila moja ilionyesha kiwango kizuri, bila kujali matokeo ya mwisho.

Wachezaji wa timu zote nne, walicheza katika kiwango cha juu na chenye ushindani kutokana na kila timu kufanya maandalizi mazuri kwa sababu ya kuhitaji kutinga fainali na hatimaye kubeba taji hilo.

Licha ya kuwapo kwa dosari chache kabla ya kuanza kwa mechi hizo, Ceasiaa wakichelewa kufika uwanjani kama kanuni za mchezo zinavyoelekeza huku benchi la ufundi la Simba Queens likilazimika kupangua kikosi kutokana na wachezaji wake baadhi wa kikosi cha kwanza ambao ni raia wa kigeni kutokuwa na vibali.

Kuchelewa kupatikana kwa vibali kwa wachezaji hao wa Wekundu wa Msimbazi kulizua sintofahamu, lakini taratibu na kanuni za nchi ziliheshimiwa mpaka pale walipopata vibali ndio wakaruhusiwa kuingia mchezo isipokuwa kocha mkuu wa timu hiyo na nyota wengine watatu, ambao nyaraka zao hazikukamilika.

Ukiondoa taratibu hizo za kiutawala, mashabiki waliofika kwenye Uwanja wa KMC Complex walipata burudani na hii inaonyesha katika msimu mpya mambo yatazidi kuwa bora kwa sababu hakuna timu ndogo au timu inayoingia uwanjani na matokeo 'mfukoni'.

Hongera kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF), Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TFF), na Kamati ya Soka la Wanawake kwa kuhakikisha kandanda kwa wanawake linaendelea kusonga mbele kadri siku zinavyokwenda.


Ni ukweli usiofichika kuwa na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania yenye ushindani, Ligi ya Wanawake Daraja la Kwanza imara na Ligi ya Mabingwa wa Mikoa yenye ubora, ndio 'kisima' sahihi kinachozalisha wachezaji wanaoitwa kwenye timu ya taifa.

Ili kuhakikisha malengo ya TFF na TWFA yanafikiwa, huu ni wakati wa mikoa kuanza pia maandalizi ya timu zao zilizoko katika Ligi Daraja la Kwanza lakini pia kuzitaka klabu zinazotarajiwa kushiriki Ligi ya Mabingwa wa Mikoa kujiweka tayari kwa ushindani huku wakihakikisha wanaendesha ligi na si kusimamia mashindano ya muda mfupi.

Mikoa inayowakilishwa na mabingwa waliotokana na michuano ya 'zimamoto' matokeo yake huonekana mapema kwa wachezaji kushindwa kwenda na kasi na kusababisha kupokea vichapo vya aibu au kuwa wasindikizaji na kushindwa kupeperusha vyema bendera za mikoa wanayotoka.

Licha ya uwekezaji katika soka la wanawake kuwa ni changamoto, hili lisiwape 'mwanya' viongozi wa mikoa kuacha kuandaa vyema timu zao na kwa kufanya hivyo itawapelekea kila mwaka washindwe kupanda daraja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Hongera Yanga Princess kwa usajili, Simba Queens jiulizeni

**JUMATANO** iliyopita niliitazama mechi ya nusu fainali ya Ngao ya Jamii ya Wanawake kati ya Simba Queens dhidi ya Yanga Princess, nikagundua baadhi ya vitu ambavyo si wengi ambavyo walivitarajia.

Kwanza kabisa wengi walidhani Simba Queens ingeshinda mechi hiyo kirahisi kama ambavyo huwa inafanya, lakini haikuwa hivyo.

Kila mmoja alijua Yanga Princess ingeteseka katika mchezo huo kutokana na wapinzani wao kuwa na kikosi bora na imara, lakini ilikuwa kinyume chake.

Mechi iliisha kwa Yanga Princess kushinda penalti 4-3, baada ya sare ya bao 1-1 dakika 90 za kawaida.

Almanusura mechi imalizike kwa bao 1-0, kama si goli la dakika za majeruhi la Mkenya, Jentrix Shikangwa.

Kwa jinsi mchezo ulivyochezwa kwa dakika zote 90, isingekuwa haki kama Yanga Princess ingepoteza, hata kwenye mikwaju ya penalti.

Ilistahili kushinda, na kweli ikashinda hata timu hizo zilipokwenda kupigiana mikwaju ya penalti.

Hata kwenye matuta pia, Yanga Princess ilistahili kushinda kwa jinsi wachezaji wake walivyokuwa makini kwenye upigaji pamoja na umahiri wa kipa wao mpya, Rita Akarekor, anayeichezea timu ya taifa ya Nigeria, akisajiliwa kutoka Delta Queens ya nchini humo.

Inaonekana ni kama viongozi wa Simba Queens hawakujiandaa vyema timu yao kuelekea kwenye mchezo huo.

Hata tukio la uchelewеshwaji wa vibali vya wachezaji wa kigeni ambao ni tegemeo, akiwamo Vivian Corazone, Elizabeth Wambui, Shikangwa, Precious Christopher na wengineo unaonyesha hivyo.

Waliingia dakika chache kabla ya mapumziko baada ya kukamilisha taratibu, lakini tayari timu ilikuwa imeshapachikwa bao. Kuingia kwao kidogo timu ilitulia.

Pamoja na matatizo hayo, ukiangalia kiwango cha Simba Queens kimepungua na si kama ilivyokuwa misimu miwili iliyopita.

Kuna wachezaji wachache sana ambao wanaweza kuibeba timu hiyo, lakini wengi kwa sasa wanaonekana wameshuka viwango.

Hata upande wa golikipa pia unaonekana kuna matatizo na linatakiwa kufanyiwa kazi haraka sana kwa kusajili kipa imara mwenye hadhi ya michuano ya kimataifa.

Pia inaonekana wachezaji ni wazito kama vile hawafanyi mazoezi ya stamina na pumzi, tofauti na wenzao wa Yanga Princess.

Nadhani tayari viongozi na wachezaji walishaanza kubweteka baada ya kuona hawapati upinzani mkubwa zaidi wanapokutana na timu moja tu ya JKT Queens.

Kiwango cha timu hiyo kilianza kutia shaka kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Kanda ya CECAFA iliyofanyika hivi karibuni huko Ethiopia, ambapo haikufanya vyema, ikipoteza michezo yake dhidi ya timu ambazo kama ingekuwa bora kama ambavyo huwa, isingefungwa.

Kinachotakiwa sasa kipindi cha dirisha dogo ifikapo Desemba, kwa kuondoa baadhi ya wachezaji wasio na tija, na kusajili wengine wanaoongeza nguvu na chachu kikosini kwa sababu wengi wanaonekana wamesharidhika.

Pongezi ziende kwa viongozi wa Yanga Princess ambao hawakuwa na makeke, wakasajili wachezaji wengi wazuri, ambao miguu yao ndiyo iliyoongea uwanjani.

Wachezaji kama Angela Chineneri, Nyabuong Jock, Arieth Udong, Agnes Palangyo, Rita, Uzoamaka Igwe na wengineo wameongeza nguvu na ubora mkubwa katika kikosi hicho ambacho kinaonekana kitaleta upinzani mkubwa katika harakati za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania msimu huu.

Vyovyote itakavyokuwa katika mchezo wa fainali leo hii dhidi ya JKT Queens, lakini msimu huu Yanga Princess imetengeneza kikosi bora ambapo kinaonekana ni tishio.

# Katibu Mkuu aagiza WMA kutekeleza maono ya Rais

**Veronica Simba,** KIBAHA

KATIBU Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, ameitaka Menejimenti ya Wakala wa Vipimo (WMA) kutekeleza maono ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuzingatia utendaji kazi wenye weledi, ubora na viwango ili kupata matokeo chanya katika sekta ya biashara nchini.

Dk. Abdallah aliyasema hayo juzi Kibaha mkoani Pwani baada ya kufungua rasmi kikao cha menejimenti ya WMA, kukabidhi magari ili kuboresha utendaji kazi na kuzindua Jarida Maalum la Wakala lenye lengo la kupanua wigo wa uelimishaji na uhabarishaji umma kuhusu WMA.

"Lengo kubwa la kikao chetu ni kukumbushana wajibu na dhamira nzima ya majukumu yetu ambayo yanatakiwa yaakisi maelekezo na miongozo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan katika suala zima la kuwezesha ufanyaji biashara ndani ya nchi yetu," alisema.

Ili kuhakikisha maono ya Rais yanafikiwa, Dk. Abdallah aliitaka WMA kuzingatia utii wa sheria, miongozo na kanuni mbalimbali zilizopo kwa kuongeza uadilifu na weledi kazini.

Pia aliwataka kufanya kazi kwa ushirikiano kama timu moja na kuwa na kauli moja baina ya bodi, mkuu wa wakala, menejimenti, viongozi wa mikoa na wafanyakazi wote kwa lengo la kupata matokeo chanya katika kazi.

Vilevile, aliielekeza Menejimenti kuondoa urasimu wa aina yoyote katika utendaji kazi huku akisisitiza kwamba jarida alilozindua pamoja na kutoa habari mbalimbali za wakala, litumike kama nyenzo ya utoaji taratibu mbalimbali zinazopaswa kufuatwa na wadau wa WMA hususani katika ufanyaji biashara.

Katibu Mkuu alisisitiza uongozi wa WMA kuzingatia yaliyomo katika Mkataba wa Huduma kwa Mteja, ambao unaelekeza kutoa huduma bora na kwa wakati.

Katika hatua nyingine, Dk. Abdallah alimpongeza na kumshukuru Rais Samia kwa kuendelea kuboresha mazingira ya utendaji kazi kwa sekta mbalimbali za umma na kwa muktadha huo kwa WMA na ametoa magari 10 kwa wakala hiyo ili kuboresha utendaji kazi.

"Leo (juzi) nimekabidhi magari mawili kwa WMA na mengine manane yako kwenye mchakato na tutayakabidhi mara moja utakapokamilika. Kwa hili, tuendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya menejimenti nzima, Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla, alisema watatekeleza maelekezo yote yaliyotolewa na Katibu Mkuu.

Kuhusu majukumu ya WMA ambayo ndiyo hasa yaliyotolewa maelekezo kuongeza nguvu, Kihulla alisema ni pamoja na uhakiki wa vipimo, ukaguzi wa vipimo na ukaguzi wa bidhaa zilizofungashwa kwa lengo la kukuza uchumi katika sekta mbalimbali.

"Lengo ni kukuza uchumi katika sekta mbalimbali lakini pia kusaidia wananchi wanaonunua bidhaa mbalimbali zinazozalishwa nchini na zinazotoka nje ya nchi, ziwe katika uzito sahihi, ujazo sahihi, urefu sahihi pamoja na namba yaani idadi sahihi," alisema.

Kuhusu magari waliyopokea, Kihulla aliishukuru wizara na kukiri kuwa yatapunguza changamoto iliyopo lakini akaomba wakala iendelee kufikiriwa kupatiwa mengine zaidi pamoja na vitendea kazi vingine mbalimbali ili kuboresha zaidi utoaji huduma kwa wananchi.

Kikao hicho cha menejimenti ya WMA ni utaratibu wa kawaida ambao wakala imejiwekea kwa kukutana kila robo ya mwaka wa fedha kujadili maendeleo ya utendaji kazi na namna ya kuboresha zaidi.

Kikao hicho cha siku tatu kilichoanza Oktoba 2, mwaka huu, kimejumuisha menejimenti kuu kutoka makao makuu na mameneja wa mikoa yote Tanzania Bara.




Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, akikata utepe kuashiria kukabidhi magari kwa Wakala wa Vipimo (WMA), ili kusaidia kuboresha utendaji kazi baada ya kufungua Mkutano wa Menejimenti ya WMA katika Shule ya Uongozi ya Mwalimu Julius Nyerere, Kibaha mkoani Pwani juzi. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa WMA, Alban Kihulla. **PICHA: WMA**

# Biteko akunwa wanafunzi mchepuo wa sayansi kusoma mazingira bora

**Na Romana Mallya**

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, ameupongeza Mfuko wa Abbott wenye malengo ya kuboresha maisha ya wananchi na kujenga jamii yenye afya njema, kwa kuwezesha wanafunzi 800 mchepuo wa sayansi kusoma katika mazingira bora.

Mfuko huo umejenga na kuiboresha Shule Sekondari ya Miles na Kimberly White iliyoko Mapatano ya mkoani Tanga ili kuwezesha wanafunzi wa kidato cha tano na sita mchepuo wa sayansi, teknolojia, uhandisi na hesabu kusoma katika mazingira rafiki.

Akizungumza katika uzinduzi huo uliofanyika Jumanne, Dk. Biteko alipongeza mfuko huo kwa namna unavyojitolea kuhakikisha sekta ya elimu inaboreka.

Shule hii ni matokeo ya ushirikiano wa muda mrefu kati ya Serikali ya Tanzania na mfuko huo wenye malengo ya kuboresha maisha ya wananchi na kujenga jamii yenye afya njema.

"Ninawapongeza wadau wote mlioshiriki kwa hali na mali hususan mfuko wa Abbott kwa namna mlivyojitolea, tunawashukuru kwa michango ambayo mmekuwa mkitoa katika jamii tangu mmekuja nchini," alisema.

Dk. Biteko aliwataka wananchi kutumia miundombinu waliyonayo sekta ya elimu kuwezesha watoto wao kupata elimu.

Mwenyekiti na Ofisa Mkuu Mtendaji wa mfuko huo, Robert Ford, alisema: "Pamoja na afya, elimu ni msingi wa maendeleo na ustawi wa jamii zetu. Ndio maana tumefanya elimu kuwa lengo kuu la ushirikiano wetu wa muda mrefu nchini."

Ford alisema wanaamini uwekezaji huo katika elimu utasaidia watu wengi zaidi nchini Tanzania kuishi maisha yao kikamilifu.

Shule hiyo ilibadilishwa jina kwa heshima ya Mwenyekiti na Mkurugenzi Mtendaji mstaafu wa Abbott, Miles White na marehemu mkewe Kimberly, ambao wametoa msaada wa muda mrefu kwa jamii za wananchi wa wilaya ya Mkinga, ikiwa ni pamoja na kujenga shule ya msingi katika kijiji jirani cha Bantu, akishirikiana na Mfuko wa Abbott.

Ili kusaidia uundaji wa shule mpya, mfuko huo ulitoa ufadhili wa zaidi ya Dola milioni nne na wahandisi wa Abbott wanatoa usaidizi wa kiufundi unaoendelea ili kuhakikisha uendelevu wa muda mrefu wa vifaa vya chuo kikuu.

Kwa zaidi ya miongo miwili, Abbott na Mfuko wa Abbott wameshirikiana na serikali ya Tanzania kuimarisha mfumo wa huduma za afya nchini na kujenga jamii zenye afya njema.

# TIC kuboresha huduma kidigitali

**Na Enock Charles**

KITUO cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kimedhamiria kutumia huduma za kijitali kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2028 ikiwa sehemu ya mkakati wa kuboresha huduma zake.

Akizungumza na vyombo vya habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TIC, Gilead Teri, alisema kwa sasa wako katika mpango wa kuwaunganisha watoa huduma za uwekezaji na wateja katika mfumo wa kidijitali ili kurahisisha huduma.

"Tunatarajia kwamba kila tunachokifanya katika kituo cha uwekezaji ifikapo mwaka 2028 kitakuwa katika mfumo wa kidijitali ili kuokoa muda, gharama na pia kufanya kazi kwa ufanisi," alisema. Alisema huduma hizo ni za simu za mkononi pamoja na intaneti katika kituo cha uwekezaji jambo linalotarajiwa kuongeza muunganiko wa huduma zinazotolewa katika ofisi za kituo hicho makao makuu na katika kanda mbalimbali.

"Kituo cha uwekezaji kina ofisi kadhaa za kanda ikiwamo Dodoma, Arusha, Mwanza, Mbeya kwa hiyo tunategemea kuziunganisha kidijitali," alisema.

Alisema ni matarajio yao kwamba matumizi ya huduma za mtandaoni yatavutia wawekezaji mbalimbali duniani kuja kuwekeza Tanzania kutokana na urahisi wa kupata taarifa kuhusu kituo hicho na usajili wa haraka wa wawekezaji.

Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh ambao wameingia makubaliano ya miaka miwili katika kuboresha huduma za Kituo cha Uwekezaji Tanzania alisema anaamini ushirikiano wao utazalisha fursa za uwekezaji.

# MOI kuhudumia wagonjwa wa nje 3,000

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Tiba ya Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI) inatarajia kuanza kuhudumia wagonjwa wa nje 1,500 hadi 3,000 kwa siku.

Hatua hiyo ni baada ya kukamilika kwa miradi mikubwa mitatu ya ujenzi wa jengo jipya ya Wagonjwa wa Nje (OPD), ukarabati jengo la Hospitali ya Tumaini na ujenzi wa Kituo cha Utengamao Mbweni.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MOI, Dk. Lemeri Mchome, aliyasema hayo juzi katika Kikao cha Tano cha Baraza la Tano la Wafanyakazi wa MOI, kinachoendelea jijini Dar es Salaam.

Dk. Mchome alisema hatua hiyo ni utekelezaji wa mipango ya serikali kupitia Wizara ya Afya wa kuhakikisha inapunguza msongamano wa wagonjwa na kuboresha huduma kwa wananchi.

Alisema miradi hiyo itaongeza idadi ya wagonjwa watakaolazwa kutoka 362 hadi kufikia zaidi ya 500 kwa siku na kuwezesha wananchi kupata huduma bora kwa wakati. Akifungua kikao hicho, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini MOI, Prof. Charles Mkony, aliwataka watumishi kuongeza ubunifu katika kutoa matibabu ili wagonjwa waweze kupona haraka na kurejea katika shughuli zao za kawaida.

"Ni lazima jamii ifahamu kuwa MOI inatoa matibabu ya kipekee kabisa tofauti na maeneo mengine, huduma zake ni za kipekee na zinahitaji ubunifu zaidi ili kuwawezesha wagonjwa kupona haraka.

"Wakati menejimenti wakiendelea na uboreshaji wa maslahi ya watumishi na miundombinu ya kufanyia kazi, niwaombe watumishi endeleeni kuwa mstari wa mbele kupiga vita rushwa, sijasikia kwa siku za hivi karibuni na ndiyo maana ninasema endeleeni hivyo," alisema.




Meneja Mwandamizi wa program maalum katika Shule ya Mtakatifu Jude ya jijini Arusha, Vivian Deus (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa Sahara Ventures, Jumanne Mtambalike, wakishiriki mjadala kuhusu changamoto mbalimbali zinazozikabili taasisi za elimu ya juu Kusini mwa Afrika wakati wa mkutano wa Umoja wa Taasisi za Elimu ya Juu Kusini Mwa Afrika, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JOHN BADI**

# Waomba ujenzi daraja kunusuru maisha nyakati za mvua kubwa

**Na Timothy Itembe,** MARA

WAKAZI wa Kijiji cha Getarungu, Kata ya Nyansurura, wilayani Serengeti, mkoani hapa, wameiomba serikali kuwajengea Daraja la Mto Nyahende, ili kuokoa maisha yao nyakati za mvua.

Akiwasilisha ombi la wananchi kwa Waziri wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora, George Simbachawene, wakati wa ziara ya kikazi wilayani hapa, Diwani wa Nyansurura, Joseph Seronha, alisema wakazi wa eneo wamekuwa wakitenganishwa na mto huo wakati wa mvua.

Alisema kutokana na kutokuwapo kwa daraja baadhi wanaolazimisha kupita husombwa na maji.

Seronha alisema pia, wananchi wamekuwa wakitembea umbali wa zaidi ya kilometa nane kufuata huduma ya afya katika kituo cha afya kilichoko Nyansurura na kuomba serikali kuwajengea kituo chao cha afya. Seronha alisema licha ya Shirika la Hifadhi ya Taifa (TANAPA) kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Ujerumani kuwajengea zahanati, bado wanauhitaji wa kituo cha afya pamoja na daraja hilo, ili kupata huduma muhimu.

Mbunge wa Serengeti, Amsabi Mrimi, alisema wananchi hasa wanafunzi wanapata shida ya kuvuka katika mto huo hasa wakati wa mvua kwa sababu shule iko upande wa pili wa kijiji hicho.

Kadhalika alisema wanahitaji kituo cha afya ili kuwanusuru maisha ya wananchi wakiwamo wajawazito na watoto.

Waziri Simbachawene alitoa miezi miwili na siku 20 daraja hilo lijengwe na kukamilika ili wananchi kupata huduma kwa urahisi.

Mganga Mfawidhi wa zahanati hiyo, Dk. Adamu Sulubila, alisoma taarifa za mradi huo wa zahanati inayojengwa na TANAPA alisema ujenzi wake unagharimu zaidi ya Sh. milioni 378.8 na itahudumia kaya zaidi ya 583 zenye wananchi 3,921 wa Kijiji cha Getarungu. Mkuu wa Mkoa Mara, Kanali Evansi Mtambi, alitoa wiki nane kuhakikisha ujenzi wa nyumba ya mganga katika zahanati hiyo uwe umekamilika.

# Wasimamizi uchaguzi waonywa udanganyifu

**Na Elizabeth Seleman,** SENGEREMA

WASIMAMIZI wasaidizi wa uchaguzi wa serikali za mitaa katika Halmashauri ya Sengerema mkoani Mwanza wamekula kiapo cha utii na uandilifu, huku wakionywa kuhusu vitendo vya udanganyifu wakati wa uchaguzi.

Kamishna wa viapo, Christopher Mbuba, Msimamizi wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa katika Halmashauri hii, Binuru Shekidele, akizungumza baada ya kiapo hicho, aliwataka kuviheshimu.

Aliwakumbusha kwamba mchakato wa uchaguzi ni muhimu na ni vyema wakafuata miongozo waliyopatiwa katika mafunzo ya awali.

Shekidele alisema hakuna msimamizi msaidizi atakayevumiliwa kwa kukiuka sheria na taratibu za uchaguzi huo na kuwa sheria kali zitachukuliwa dhidi yao.

Binuru alisema iwapo wasimamizi hao watafikisha elimu sahihi kwa wapiga kura hakutakuwa na upotoshaji na wananchi wengi watajitokeza kujiandikisha ili kupiga kura.

# Nyumba kaya nne yateketea kwa moto

**Na Steven William,** MUHEZA

NYUMBA yenye kaya nne iliyoko Mtaa wa Majengo, Kata ya Majengo, wilayani Muheza Tanga, imeteketea kwa moto huku vilio vikitawala.

Tukio hilo limetokea juzi mchana katika eneo hilo na hivyo wananchi kujaa kwa ajili ya uokoaji vifaa ndani ya nyumba kwa kushirikiana na Askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji.

Kaimu Mkuu wa Zimamoto na Ukoaji Wilaya ya Muheza, Sajenti Mwanshasha Mhina, alisema nyumba hiyo iliyoteketea kwa moto ilikuwa inamilikiwa na Sadiki Fatee.

Alisema nyumba hiyo ilikuwa na kaya nne lakini zilizoteketea kwa moto zilikuwa tatu zenye jumla ya watu wanane.

Mhina alisema katika tukio hilo kati ya vyumba saba, vitano vimeteketea kwa moto na viwili vimenusurika.

Kwa mujibu wa Mhina, chanzo cha moto huo bado hakijafahamika na kwamba uchunguzi unaendelea japo kuwa wanahisi ni gesi.

Alisema waliwahoji wakazi wa nyumba hiyo, Zubeda Seif mwanafunzi wa darasa la tatu na Catherine Malya, kuhusu tukio hilo na kubainisha kuwa ndani wanatumia jiko la gesi.





# Magereza yapokea magari ya mahabusu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JESHI la Magereza limepokea magari 11 huku likitarajia kupokea mengine 17 ili kuondokana na changamoto ya usafiri wa kubebea mahabusu kuwapeleka mahakamani.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Ally Gugu, alisema magari hayo na mengine ambayo yataendelea kuletwa, yamenunuliwa kwa fedha za bajeti ya Mwaka 2023/24, Sh.bilioni 6.2 iliyotolewa na serikali kwa ajili ya ununuzi wa magari ili kukidhi mahitaji yaliyopo.

Alisema magari 10 ambayo yamewasili yatatumika katika shughuli za kiutawala na mengine 17 yatakayoletwa yatatumia kusafirisha mahabusu.

Gugu aliwasihi kuhakikisha magari hayo yanatunzwa ili kudumu kwa muda mrefu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za urekebu za jeshi hilo.

Naye Mkuu wa Jeshi la Magereza nchini, Kamishna Jenerali Jeremiah Katungu, aliishukuru serikali kwa kutoa fedha hizo za kununua magari hayo.

Alisema magari yatagawiwa na magereza mbalimbali na gari moja la wagonjwa litapelekwa Hospitali ya Ukonga Magereza ili kusaidia utoaji huduma.

"Naishukuru sana serikali kutokana na fedha ilizotupatia magari haya yatatumika ipasavyo kwa ajili ya shughuli za magereza," alisema.

Kamishna Jenerali Katungu alisema jeshi hilo linaendelea na utekelezaji wa shughuli za magereza ambazo zinafanyika kiweledi ili kuhakikisha kila magereza inakuwa sawa.

# Bashungwa ataja mwarobaini ajali barabarani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Ujenzi, Innocent Bashungwa, amesema katika kutekeleza mkakati wa kupunguza ajali nchini, mpango wa serikali ni kujenga barabara za njia tatu kwenda na kurudi katika maeneo mbalimbali nchini.

Bashungwa alisema hayo juzi wakati wa ziara ya kukagua utekelezaji wa ujenzi wa barabara ya mzunguko yenye urefu wa kilometa 112.3 katika jiji la Dodoma, inayotarajiwa kukamilika Machi, mwakani.

Alisema mpango wa serikali hivi sasa ni barabara ambazo zitakuwa zikijengwa katika maeneo mbalimbali ya nchi kuwa za njia tatu ili kusaidia kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea.

"Mpango wa serikali hivi sasa ni ujenzi wa barabara kuwa za njia tatu kwenda na kurudi na kuondokana na ujenzi wa sasa magari kupisha katika njia moja. Mpango wetu hata hizi barabara ambazo tunazitumia sasa zikibadilishwa zitakuwa za njia tatu ili kusaidia kupunguza ajali nchini," alisema Bashungwa.

> **"Serikali haitaongeza hata siku moja ya ziada, hivyo mnapaswa kukamilisha ndani ya muda wa mkataba na mkandarasi atakayeshindwa serikali haitampatia kazi nyingine**

Kuhusu ujenzi wa barabara ya mzunguko ya kilometa 112.3, aliwataka makandarasi kumaliza ndani ya muda wa mkataba kwa kuwa serikali haitaongeza hata siku moja ya ziada.

"Serikali haitaongeza hata siku moja ya ziada, hivyo mnapaswa kukamilisha ndani ya muda wa mkataba na mkandarasi atakayeshindwa serikali haitampatia kazi nyingine tena kwani kuongeza muda ni kuongeza pesa, hivyo serikali haitakuwa tayari kufanya hivyo," alisema.

Msimamizi wa Miradi kutoka Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mhandisi Faustin Laswai, alisema ujenzi wa mradi huo umegawanyika katika vipande viwili na mkandarasi wa kwanza anatekeleza kipande cha urefu wa kilometa 52.3.

"Mkandarasi wa pili anatekeleza kipande cha urefu wa kilomita 60 na ujenzi huu ulianza Septemba, 2021 na umepanga kukamilika Machi, 2025," alisema.

Hata hivyo, alisema hadi sasa mradi huo kipande cha kwanza kimekamilika kwa asilimia 83.66 na kipande cha pili asilimia 79.1 ambapo wanatarajia kukamilika ndani ya muda wa mkataba Machi,2025.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Mhandisi Hamad Masauni (katikati), akizungumza na wananchi baada ya kuzindua jiwe la msingi la ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Daraja B, wilayani Chemba, mkoani Dodoma, jana. **PICHA: MAULID MMBAGA**

# Mfumo stakabadhi ghalani wanufaisha wakulima

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MFUMO wa stakabadhi ghalani umeleta manufaa makubwa kwa wakulima wa dengu mkoani Singida na kwa kipindi cha miezi miwili, zaidi ya Sh. bilioni 25 zimezunguka kwa wakulima waliouza zao hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, aliyasema hayo juzi kwenye kikao cha kufanya tathmini ya utekelezaji wa mfumo huo katika msimu huu wa kilimo.

"Singida tumetekeleza kwa mafanikio makubwa kwa muda mfupi wa miezi miwili hadi mitatu zaidi ya Sh. bilioni 25 zimezunguka kwa wakulima, hivyo tuna kila sababu ya kuipongeza serikali kwa kuweka mifumo rahisi ya wakulima wa nchi hii kupata stahiki zao zinazostahili," alisema.

Dendego alisema mkoa wa Singida hautarudi nyuma katika kuuza mazao kwa kutumia mfumo huo licha ya kuwapo na kero mbalimbali.

Alisema kwa mabilioni yaliyopatikana kwa wakulima kutokana na kuuza Dengu hakuna sababu ya kuuita mkoa huu ni maskini bali imejionyesha kuwa fedha zipo ila zilikuwa hazijaratibiwa vizuri.

"Nani leo alitegemea dengu italeta Sh. bilioni 30 hapa? Ilikuwa inauzwa lakini kwa sababu ilikuwa hairatibiwi vizuri ndiyo maana ilikuwa haionekani kama Singida inazalisha dengu kwa wingi," alisema.

Dendego alisema iwapo mfumo huo utatekelezwa katika mazao mengine kama pamba, tumbaku, vitunguu, alizeti na mahindi, hakutakuwa na umaskini Singida.

"Kwa hiyo Singida lazima safari hii tupindue meza na safari imeanza. Lazima tushirikiane na maafisa ushirika kuanzia ngazi ya mkoa hadi wilaya. Mwelewe kipenga kimelia zile chengachenga mimi sizitaki. Tukisimama wote hakuna atakayetushinda.

"Mtu yeyote atayetaka kukwamisha utaratibu wa uuzaji mazao kwa kutumia mfumo huo atashughulikiwa kwa kuwa lengo la serikali ni kila mtu apate haki yake kulingana na jasho lake.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, aliwataka maofisa ushirika kutoa elimu kwa wananchi ili kuufahamu mfumo huo.

Dk. Mganga alitaka suala la usimamizi wa fedha zinazotokana na mfumo huo liwekewe utaratibu mzuri ili kuepusha malalamiko ya wakulima hasa wanapocheleweshewa malipo.

Septemba 7, mwaka huu, wafanyabiashara wa mazao na makuli wa mizigo mjini Singida waliandamana na kufunga barabara kuu ya Dodoma-Singida-Shinyanga kwa magogo na miti wakipinga mfumo huo. Mkoa wa Singida ulizindua rasmi utekelezaji wa mfumo huo kwa msimu 2024/25 kufuatia maagizo yaliyotolewa na serikali kupitia mwongozo wa biashara ya zao la dengu, mbaazi na ufuta.

Mwongozo huo ulitolewa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA),Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC),Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa (TMX).





## SMZ yazuia matumizi ya mawe katika ujenzi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imezuia matumizi na usafirishaji wa mawe katika shughuli za ujenzi kwa sababu mbalimbali ikiwamo ya hali ya mazingira.

Waziri wa Maji, Nishati na Madini, Hassan Shaibu Kaduara, alisema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari huko ofisini kwake Maisara visiwani Zanzibar.

Alisema uamuzi huo umefikiwa kutokana na uharibifu wa mazingira unaoendelea serikali ikaamuwa kupiga marufuku juu ya matumizi ya rasilimali hiyo.

Waziri Kaduara alisema kuwa katazo hilo limeangalia maslahi mapana ya taifa hivyo kila mwananchi anatakiwa kufahamu kuwa athari za kimazingira ni kubwa kuliko faida inayopatikana katika rasilimali hiyo.

"Serikali imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya athari za kimazingira juu ya rasilimali ya mawe inavyo athiri mazingira," alisema Kaduara.

Alisema katika kipindi hiki cha katazo, ni vyema wananchi kutumia matofali kwa ajili ya msingi na utafiti uliyofanywa kutumia matofali ni rahisi kuliko kutumia mawe kwa ajili ya kujengea.

Waziri huyo alisema kuwa viwanda vinavyojishughulisha na uzalishaji wa kokoto kufanya shughuli zao katika maeneo yenye mawe ili kuendelea kutoa huduma za kokoto kwa wananchi wa visiwa wa vya Zanzibar.

Serikali, alisema imefikia uamuzi huo kutokana na uharibifu mkubwa wa mazingira pamoja na kuharibiwa kwa maeneo ya wananchi na serikali kwa kuzuia mawe.

Alisema serikali imekuwa ikipokea malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya athari wanazozipata kutokana na uwepo wa viwanda vya kusagia mawe katika maeneo ya makazi.

"Kumekuwa na malamamiko mengi wananchi wakiyatoa juu ya kuwepo mitani viwanda hivyo na sisi kama serikali tukaono kufanya uwamuzi huo," alisema Kaduara.

Alisema kuendelea kuwapo mitaani kwa viwanda hivyo ni moja ya kuondosha hata haiba ya Zanzibar kwa vile visiwa hicho ni maarufu katika shughuli za utalii.

# Mwinyi ataka hatua madhubuti kero zilizojadiliwa kuhusu afya

**Na Rahma Suleiman,**
ANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema changamoto zote zilizojadiliwa katika kongamano la 11 la Tanzania Health Summit lililofanyika visiwani Zanzibar, zinahitaji kuchukuliwa hatua madhubuti na za haraka.

Aliyasema hayo wakati akifunga kongamano hilo lililofanyika katika viwanja vya biashara Nyamanzi, mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja.

Dk. Mwinyi alisema kongamano hilo si jukwaa la majadiliano bali pia ni chombo cha kuchochea utekelezaji wa mipango mbalimbali ya kuimarisha afya za wananchi.

Alisema serikali inaendelea kuunga mkono jitihada hizo na iko tayari kushirikiana na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sekta binafsi na washirika wa maendeleo ili kufikia malengo ya afya bora kwa wananchi wote.

Rais Mwinyi alisema lengo ni kuondoa changamoto ikiwamo kupunguza vifo vya mama na mtoto, kuhakikisha upatikanaji wa dawa muhimu, uimarishaji wa miundombinu ya afya, upatikanaji wa taarifa za afya, udhibiti wa maradhi ya kuambukiza na yasiyo ya kuambukiza na mengineyo.

"Ndugu washiriki wa kongamano na wageni waalikwa, ni matumaini yangu kuwa maazimio na mapendekezo yaliyotokana na kongamano hili hayataishia hapa, bali yataendelea kuwa mwongozo muhimu katika kuimarisha sekta ya afya nchini," alsiema Dk. Mwinyi.

Pia alisema ni lazima kuyatekeleza kwa dhati, kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi katika kuwahudumia Watanzania wote kwa misingi ya usawa na haki.

**"Ni mategemeo yangu kwamba kupitia mafunzo haya pamoja na mambo mengine, lakini pia yataongezea ujuzi na ubunifu utakaowaongoza kufanya kazi zenu kwa mujibu**

Aliitaka Wizara ya Afya Zanzibar kuchukua mapendekezo hayo na wayafanyie kazi ipasavyo katika utekelezaji wa mipango kazi yake inayoiandaa kila mwaka. Waziri wa Afya Zanzibar, Nassor Ahmed Mazrui, alisema kongamano hilo lilichanganua changamoto za afya na liliwakutanisha wabobezi wa masuala ya afya kwa lengo la kuimarisha huduma za afya za msingi nchini.

Alisema mkutano huo kufanyika Zanzibar ni chachu ya huduma bora za afya kwa kuhakikisha huduma za afya zinafika kuanzia katika vituo vidogo na hospitali za wilaya na rufani.

Mazrui alisema serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha huduma za afya katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha Wazanzibari wanapata huduma bora za afya.

Aliwataka washiriki wote kuyatumia mafunzo hayo kama kiungo muhimu cha kuboresha huduma za afya nchini na kuwataka ambao hawajaanza kufanya tafiti za afya kuanza kwasababu zimeonesha mafanikio makubwa na kutatua changamoto mbalimbali.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya Zanzibar, Dk. Miraji Mngereza, alisema mkutano huo umeleta mafanikio makubwa kwa kujadili mipango mbalimbali ya maendeleo yaliyolenga watoa huduma wakiwamo viongozi wa tiba ili kuendana na mabadiliko. Rais wa Tanzania Health Summit, Dk. Omar Chillo, aliitaka serikali kuendelea kufanya kazi kwa pamoja kwa lengo la kuleta mabadiliko katika sekta ya afya Tanzania.



Rais wa Chama cha Madaktari Wanawake Tanzania (MEWATA), Dk. Zaitun Bokhary (wapili kushoto), akipeana mikono na Daktari Bingwa wa Kinamama wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, Hassanat Abdallah, wakati Mewata na Chama cha Madaktari Wanawake Zanzibar walipokutana na kuunganisha nguvu, jijini Zanzibar mapema wiki hii na kupokea wanachama wapya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Othman: Zanzibar mwasisi wa uhifadhi mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema kihistoria Zanzibar ilikuwa mstari wa mbele Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Othman aliyasema hayo katika maeneo tofauti kwenye ziara yake maalum ya ukaguzi wa maeneo ya miradi ya uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani katika mkoa wa Kusini Pemba.

Alisema uoto wa asili, ukijani wake na misitu, ulisaidia kuipendezesha na kuitangaza Zanzibar, sambamba na kusaidia malezi ya watoto wa visiwa vya Unguja na Pemba na ilikuwa chanzo cha chakula chao cha kawaida.Kuhusu mpango wa kitaifa wa kuirithisha Zanzibar ya kijani mbele ya viongozi, wamazingira, watendaji wa sekta mbalimbali na wananchi, Othman alisema dhamira ni kutekeleza dhana kuwa mazingira ni uhai, mazingira ni uchumi, na ni sehemu muhimu ya maisha ya mwanadamu katika kujiletea maendeleo.

"Jambo la msingi lazima tutambue kuwa tumeharibikiwa na mazingira, matumizi ya maji na ardhi nayo yameongezeka kutokana na mahitaji pamoja na kasi ya ongezeko la watu. Ni wajibu sasa turudishe miti ya baharini, pamoja na ya nchi kavu na ndiyo maana tumeleta mpango huu", alisema.

Akizungumzia uharibifu, uvamizi na wizi wa misitu ya asili, Othman alisema suluhisho la udokozi huo, mbali na kuwafikisha wahusika mbele ya vyombo vya sheria, ni vyema kuongeza kasi ya uzalishaji na uhifadhi wa mazingira.

Pia aliwataka watendaji kuwa na mtazamo wa mbali na wasichukulie suala la mazingira kama jambo la kawaida, bali wahakikishe kasi ya uchimbaji wa ardhi na ukataji wa miti inaendana na kasi ya urejeshaji, ili kuwapo mipango bora na endelevu, kwa ajili ya kufanikisha mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani. "Tunayo mifano mingi ya nchi za wenzetu na ni wajibu wetu kushirikiana na jumuiya na taasisi zingine kama Mamalaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) na hata baadhi ya NGO ili kufanikisha dhamira hiyo", alisisitiza.

Alisema Zanzibar haina budi kujifunza kwa visiwa vya Mauritius na Shelisheli ambavyo vimefanikiwa kukuza uchumi kupitia uhifadhi na utunzaji wa mazingira.

Hata hivyo, alitaka jamii kuendeleza utamaduni wa kuwahusisha watoto na kuwajengea uelewa juu ya thamani ya misitu na kusaidia kufanikisha kwa pamoja mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.

"Wito wangu kwenu ni pamoja na mambo mawili muhimu. Ni vyema tukatanua maeneo ya uhifadhi kwa kadiri hali itakavyoruhusu na pia wahusisheni watoto waelewe kwamba misitu ni jambo la thamani kwa maisha yao. Tukiwarithisha hayo, nao pia watakuwa wahifadhi na walinzi wa mazingira yetu," alisema.



**PROF. J**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE

JUMAMOSI OKTOBA 5, 2024



# Huyu ndiye mke wa Diamond sasa

SANURA Kasimu, ambaye ni mama wa msanii nguli nchini na Afrika kwa ujumla, Naseeb Abdul maarufu kama Diamond Platnumz, amefunguka kuwa anataka mwanaye huyo aoe mke ambaye ni mcha Mungu na atakayeipenda familia yake.

Sanura, ambaye anajulikana zaidi kama mama Dangote, amesema hata Diamond anajua anavyotamani kupata mkwe wa aina hiyo.

Alisema hayo katika sherehe ya siku ya kuzaliwa ya Diamond, ambayo hufanyika kila Oktoba 2, ambapo mwaka huu ametimiza umri wa miaka 35.

Diamond alizaliwa Oktoba 2, 1989, maeneo ya Tandale jijini Dar es Salaam na mpaka sasa bado hajafunga ndoa yoyote, lakini mama yake sasa anatamani iwe hivyo. Hizi zilikuwa ni salamu za 'bethdei' za mama kwa mwanawe.

"Maombi yangu ni kwamba aoe ili aweze kupata maendeleo. Maendeleo gani unaweza kupata bila kuoa na kuishi na mwanamke? Aoe, yeye ni mwanaume?" Nanatamani Diamond aoe na kuishi angalau na mtu, nataka mwanamke anayemcha Mungu kwa ajili ya mwanangu, mtu atakayependa familia yetu, mwenyewe anajua hili," alisema mama Dangote.

## BASI SAWA

### Vibe la Mbeya kwa Zuchu lilizidi

Meneja wa msanii Zuchu, Yekimu amebainisha kuwa anadhani fujo ya mashabiki iliyotokea Mbeya hivi karibuni ilitokana na mashabiki kuwa na vibe kupitiliza.

Yekimu ambaye yupo kwenye menejimenti ya WCB, amesema hakuwa na mchangamoto yoyote, au msanii kusema kitu chochote kibaya ambacho kiliwaudhi mashabiki jijini Mbeya.

Wiki iliyopita mashabiki wa muziki jijini Mbeya, walionekana kurusha chupa na vitu vingine hatarishi jukwani kiasi cha kumfanya msanii huyo kusitisha kuimba katika moja ya maonyesho jijini humo.

"Ni vurugu tu, walirusha chupa, hakukuwa na changamoto yoyote, labda alisema maneno fulani au kuwaudhi, ni vibe tu lilipitiliza na hii siyo kwa Zuchu tu, inawatokea wasanii wengi duniani wakiwa jukwaani, siyo kwamba alifanya vibaya, au kuna kitu kibaya alisema, hapana," alisema Yekimu.

Hata hivyo, alisema siku iliyofuata alikwenda kuwasalimia wananchi wa Mbeya na akafanya shoo nyingine iliyobamba kinoma.

### Mganga wa Dulla Makabila mkali

Msanii wa maarufu wa muziki wa singeli, Dulla Makabila amejigamba kuwa mganga wake ni mzuri, ndiyo maana kwa sasa ana mafanikio ya muziki na kimaisha pia tofauti na zamani.

Makabila ambaye anajiita mfalme, amesema huwezi kujiita hivyo bila kuwa na mganga mzuri.

"Huwezi kujiita mfalme lazima uwe unatoa nyimbo ambazo zinakaa namba moja kwenye jedwali, unawakalisha chini hata ngoma za bongo fleva, tena zilizopigwa na wasanii wakubwa, yaani kila kitu lazima uwe nacho hata mganga mzuri unatakiwa uwe naye, hutakiwi kulegalega," alisema huku akiangua kicheko.

Makabila ameongea maneno hayo, kufuatia kutoa ngoma yake tata aliyoiita, 'Tuzo', ambayo imekuwa 'inatrendi' kwenye mitandao na majukwa ya muziki.

"Sasa hivi kipesa niko vizuri, nina gari, nataka niongeze ya pili, yaani wiki hii hii nitanunua lingine, nyumba ndiyo niko katika harakati ya kujenga," alisema.



## MKE WA PROFESA JAY AMSUBIRI MUMEWE

MKE wa lejendali wa muziki wa hip hop nchini Profesa Jay, aitwaye Grace Mgonjo, amesema mpaka sasa hajajua anawaza nini kichwani mwake kama atarudi kwenye muziki, siasa au vyote kwa wakati mmoja.

Hii ni baada ya mwanzilishi huyo wa muziki wa kizazi kipa nchini kuposti video alionyesha hali aliyokuwa nayo kipindi anaumwa. Mbali na muziki, Jay, ambaye jina lake halisi ni Joseph Haule, aliwahi pia kuwa Mbunge wa Jimbo la Mikumi.

"Maisha ya Jay kwa sasa yapo na Mungu, sana sasa sijajua yeye kichwani mwake anawaza nini lakini vitu vyake vipo kama kawaida kama muziki, siasa, mambo ya jimboni, vitu vingi vinarudi kwenye kuwa kama kawaida ila Mungu yuko mbele zaidi kwake," alisema mke wa nguli huyo na kuongeza.

"Ameposti ile picha maana ameuona ukuu wa Mungu ndio maana akataka watu wajue, kwa maana wengine hawakuwa wanafahamu ameumwa kwa kiasi gani na yapi amebayo amepitia," amesema Grace.



## Dully Sykes hataki mazoea

Msanii mkongwe wa bongo fleva nchini, Dully Sykes, amebainisha kuwa ameshawahi kuwapiga 'block', kwenye mitandao yake ya kijamii, wasanii wakubwa kama Ali Kiba, Harmonize na Diamond Ptatnumz huko nyumba, ingawa kwa sasa ni washkaji zake.

Alisema mara nyingi yeye huwa hapendi dharau zinazofanywa na baadhi ya vijana wapya wanaochipukia kwenye tasnia ya muziki wa bongo fleva, hivyo akiona wanamzingua anaondoa kwenye mtandao wake.

Tayari msanii huyo ameachia ngoma yake iitwayo 'Super Star', ambayo imeanza kuwa gumzo la nchi.

"Nafanya hivyo ili kuepuka 'stresi', kutokana na dharau za vijana," alisema msanii huyo.

## MKANDALA LUFUFU HADI JUMA KHAN

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuzitazama filamu nyingi za Kizungu, Kihindi, Kikorea, Kichina na hata Kinigeria zenye lugha ya kwao kwa miaka mingi, mwanzoni mwa miaka ya 1990 vijana wengi wa Kitanzania walipata fursa ya kuanza kuzisikia zikitafsiriwa kwa kiswahili.

Filamu nyingi za miaka ya mwanzoni ya 1970 hadi mwishoni mwa miaka ya 1980 ambazo zivuma mno, zilianza kutafsiriwa kwa kiswahili na kuzidi kuzipa umaarufu.

Hata zile mpya zilizotoka miaka ya 1990 hadi sasa zimekuwa zikitafsiriwa kwa lugha ya kiswahili, hivyo kuleta mvuto na kupendwa na Watanzania wengi kwa sababu wanakuwa wanakifahamu kinachozungumzwa na maudhui ya filamu yenyewe.

Kwa sasa hata tamthilia zimekuwa zikitafsiriwa kwa lugha adhimu ya kiswahili.

Leo tutawaangalia Watanzania maarufu ambao wamekuwa wakiweka maneno ya kiswahili kwenye picha hizo.

**Mkandala Lufufu**

Anaitwa Kepteni Dereck Gasper Mukandala Lufufu. Huyu ndiye mwanzilishi au mwasisi wa kutafsiri filamu za nje ya nchi kwa lugha ya kiswahili hapa Tanzania. Ni kepteni wa Jeshi la Wananchi mstaafu ambaye alifariki dunia 2015 jijini Dar es Salaam na kuacha majonzi makubwa kwa watu wengi wapenda filamu na tamthilia, hasa ikikumbukwa kuwa ndiyo wakati tasnia hiyo ilikuwa inakuwa kwa kasi biashara hiyo ikichanganya sana kutokana na kukua kwa teknolojia, lakini pia watu wengi kuwa na uwezo wa kumiliki TV.

Hakuna kijana au mtoto yeyote wa miaka ya 1990 mpenda picha ambaye hamtambui. Watoto waliomba pesa kwa mama zao na kwenda kwenye vibanda vya video maarufu kama 'vibanda umiza' kwenda kuangalia filamu alizoweka maneno ya kiswahili kama yeye mwenyewe alivyokuwa akisema, hasa ikizingatia wakati huo bado nyumba nyingi zilikuwa hazina TV. Nakumbuka wakati huo kiingilio ilikuwa ni Sh. 50 tu.

Alitafsiri filamu za aina zote kwa umahiri mkubwa, lakini pia anakumbukwa kwa mbwembwe, kuiga sauti za wahusika wote ndani ya filamu, awe mwanaume, mlevi, aliyejeruhiwa kwa kupigwa, mwanamke mtu mzima, msichana, tajiri, masikini, kila mmoja alimtafutia sauti yake na ikawa burudani tosha. Alitengeneza maneno na misamiati mingi kwenye filamu zake kama 'kukotola' (kukimbia), 'kanyampasila', (rumande), 'kanyabazongo (kizunguzungu), bastola aliita 'mguu wa kuku.' Hakuwa mtafsiri tu, bali ni mshereheshaji 'muvu'. Jamaa ana mambo mengi sana ambayo unaweza kumaliza makaratasi yote kumwelezea. 'Akamwaga mwaaani' akiwa na maana akaanza kupiga risasi.

**Juma Khan**

Ndiye mtafsiri anayependwa zaidi na mashabiki wengi wa picha za kihindi zilizotafasiriwa kwa kiswahili. Hii inatokana na labda kufahamu vizuri lugha hiyo kwa ufasaha kutokana na utundu wake, pamoja na kupitia mikononi mwa watu wenye asili hiyo wakati akitafuta mafanikio kwenye kazi hiyo.

Pamoja na hayo, huyu jamaa amekuwa akiweka nakshi nyingi na mbwembwe zilizovutia wengi, ikiwamo misemo kadhaa.

Msemo ni 'mwamba huyu hapa', umebiniwa na mwamba huyu na mpaka sasa unatamba kwenye nyanja mbalimbali za michezo, hususan mpira wa miguu na burudani. Ni msemo ambao kwa sasa umetawala kila kona.

Juma Khan au Chikongwe hana mpinzani kwenye hili kwa sababu mashabiki wengi wa filamu hizo, wanasema picha yoyote ya kihindi iliyotafsiriwa kwa kiswahili kama aliyefanya kazi hiyo siyo huyo basi ni kama pilau bila kachumbari.

**DJ Msati**

Huyu naye anatafsri sana filamu za kihindi na tamthilia zake, anakuja juu kwenye kazi hiyo. Ni mmoja wa watafsiri anayejizolea mashabiki wake kila kukicha ambaye ni maarufu kwa jina na 'baba la baba.'

**DJ Murphy**

Ni mtafsiri kutoka Arusha ambaye anatafsiri picha zote za Kizungu, Kikorea, Kijapani na nyingine nyingi. Naye amejizolea sifa kubwa kutokana na aina yake ya kutafsiri akiwa na sauti nzito kuliko yeye mwenyewe alivyo.

**DJ Macky**

Huyu ni mtaalamu wa kutafsiri zaidi filamu za Kichina na Kivienam. Jamaa ukimsikiliza sana ni kama anamuiga Mkandala Lufufu, kwani kama ukisikia haraka haraka sauti kama zinafanana hivi.

## FILAMU

## Kiapo cha uvumilivu hiki hapa

**Na Adam Fungamwango**

WENYE moyo wa kuweza kuvumilia hadi mwisho ndiyo wanaofanikiwa. Ni msemo wa enzi na enzi. Hutumika kuwafanya watu wasikate tamaa licha ya magumu wanayopitia.

Pamoja na kwamba ndoa ni tukio jema la heshima, kiasi kwamba binadamu wengi kutaka kuwa nayo kwenye maisha, lakini huhitaji umakini, ujasiri, uimara wa kiakili na uvumilivu.

Kuna watu wanapenda ndoa kwa sababu tu ya hafla tu au sherehe zinazofanyika pale. Wengine tamaa tu za kimwili. Ukweli ndoa ni zaidi ya hivyo. Kuna wakati ukiwa ndani unaweza kujuta na kudhani ndiyo kitu kibaya zaidi duniani kuwapo. Lakini ukivumilia hadi mwisho na kuyashinda majaribu yote, ndiyo utaona utamu na raha ya ndoa.

Tuiangalie ndoa kwenye filamu ya 'Kiapo cha Uvumilivu'. Imechezwa na wasanii Nassor Bakari, Angel Mjema, Amly Amily, Margareth Emmanuel, Sutlan Mohamed, Michael William na wengineo.

Chobi na mkewe Karata wameoana kwa lengo la kufurahia ndoa yao hadi mwisho wa maisha yao. Baada ya mwaka mmoja hali ikaanza kugeuka. Ni baada ya Karata kupata ujauzito mara tatu, lakini zote inatoka kwa namna ya kushangaza.

Kutopata mtoto kunamfanya mama Chobi na ndugu zake kuanza kumsakama Karata na kumpa kila aina ya majina mabaya. Mwanzoni Karata alipata ulinzi kutoka kwa mumewe Chobi, hata hivyo kadri siku zilivyodizi kusonga mbele, mume naye alichoka kumtetea mkewe. Naye akawa anataka mtoto.

Mke ananyanyaswa, akawa kama hausigeli badala ya mke. Ni matusi, kejeli na dharau. Akaenda kwa wazazi wake kushtaki. Wazazi wakamwambia aje na mumewe. Chobi akakataa kwenda na kuzidi kumtesa mkewe.

Rafiki yake mmoja alimshauri Chobi aende kwa mpiga ramli labda kuna namna. Na kweli, mpiga ramli akamwambia kuwa mama yake mzazi ndiye anayefanya yote haya kwa sababu amejiingiza kwenye chama cha wachawi.

Lakini vile vile hata upande wa mwanamke pia kuna tatizo, ndiyo maana mke anapata ujauzito, lakini unatoka muda si mrefu.

Aliporudi alimwambia mkewe sasa amekubali kwenda ukweni kuwasikiliza. Alipofika aliomba msamaha kwa yote aliyoyafanya na kudai amegundua kuna tatizo.

Chobi pia akaenda kwa mama yake mzazi na kumweleza ukweli kuwa amegundua kuwa anahusika kwa kumfunga mkwewe ili asizae kwa sababu ya kishirikina, hivyo amfungue na kuachana na mambo ya uchawi.



Familia zote mbili zinaweka mambo sawa na Karata sasa anapata ujauzito wa nne, ambao anajifungua mtoto wa kwanza wa kike, amani, utulivu, na furaha ya ndoa inarejea kama zamani.

# Cardi B aendelea kuchafuka



WAKATI akiendelea na mchakato wa kuomba talaka, rapa mkali wa Marekani, Cardi B, amemwelezea mume wake Offset, kuwa ni muongo na amemchoka kutokana na tabia yake.

Cardi B ametumia ukurasa wake wa Instagram akielezea jinsi mwanamume huyo alivyokuwa mdanganyifu na kwamba hatarajii kurudi tena kama ilivyokuwa huko nyuma.

"Nimekufanya uonekane mzuri, sijali kuhusu wanawake wanaowatania. Sitaki kuwaona kwa sababu ungewachumbia na unachotakiwa kufanya ni kulewa na kunidanganya nimechoka," amesema Cardi B.



## Ify asimulia mazito ugumba

MTAYARISHAJI maarufu wa vipindi vya mapishi nchini Nigeria, Ify amefunguka kuwa ilikuwa maisha magumu ndani ya miaka tisa ambayo alikuwa akisaka mtoto.

Akizungumza wakati wa mahojiano ya hivi majuzi, Ify amesema katika kipindi hicho alipitia misukosuko mingi pamoja na kuumia kihisia jambo lililomsababisha kuwa na msongo wa mawazo.


"Haikuwa safari nzuri hata kidogo, linalokusumbua sana wakati wa kusubiri ni kwamba hujui lini utapata mtoto, mtu atakuja kwako kukuambia kuwa utajifungua baada ya miaka saba au minane lakini hujui lolote," amesema.

## Spyro ukitulia kumbe...

MWANAMUZIKI wa Nigeria Spyro, amewashauri wanaume waliooa kuhakikisha wanatoa matunzo mazuri kwa wake zao kwa sababu waliobaki nje sio wazuri.

Msanii huyo ameandika kupitia ukurasa wake wa Instagram kuwa ni muhimu kwa wanaume kuthamini wenzi wao na endapo atamtunza na kuwekeza kwake atagundua kuwa yeye ni mzuri kuliko wasichana waliokuwa nje.

Spyro aliongeza kwamba kuna umuhimu wa kukuza na kuthamini uhusiano wa kimapenzi, badala ya kushawishiwa na sura za wanawake wengine.





## Usher acha kuwazingua mashabiki

BAADA ya watumiaji wa mitandao ya kijamii kupatwa na hofu kufuatia kufutwa kwa akaunti ya X (zamani Twitter) ya mwimbaji wa Marekani Usher, hatimaye msanii huyo ameibuka na kudai mtandao wake ulidukuliwa.

Usher kupitia ukurasa wake wa X, amesema wadukuzi walifuta data zote baada ya kufanikiwa kuishikilia kwa muda.

"Akaunti ilidukuliwa, waliyekimbia nayo! Tuonane usiku wa leo huko Intuit Dome," ameandia Usher.

Hata hivyo, wafuasi wake wengi wa mitandao ya kijamii walisisitiza kwamba hawaamini madai yake.

## Rema akataa ushetani

MWIMBAJI wa Afrobeat kutoka Nigeria, Rema, amesema kuwa watu wanaomuhusisha na imani ya kishetani kutokana na video zake za muziki kuwa za kustaajabisha na ubora wa kazi zake.

Rema alikanusha madai hayo na kuyataja kama kichaa ambacho amewahi kujionea. Alifafanua kuwa taswira na rangi zinazotumiwa katika kazi yake ni chaguo za kisanii tu na hazihusiani na ushetani.

"Jambo la kichaa zaidi ambalo nimeona mtandaoni kuhusu ninamwabudu shetani, sio muhimu kujibu madai hayo nahisi ni kupoteza muda. Wakati mwingine ni rangi tu ambazo mimi na timu yangu tunatumia kwenye picha," amesema.



# Polisi yaendelea kumsaka muuguzi aliyetoweka

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

MAKACHERO wa Jeshi la Polisi, mkoani Kilimanjaro, bado wanahaha kumsaka Muuguzi wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Kaskazini (KCMC), Lenga Masunga (38), aliyetoweka katika mazingira ya kutatanisha Julai 2, mwaka huu.

Jana, Kamanda wa Polisi mkoani humo, Kamishna Mwandamizi Msaidizi (SACP), Simon Maigwa, aliiambia Nipashe katika mahojiano maalum kuwa, hadi sasa simu za mkononi za Masunga, hazipatikani.

Alisema katika uchunguzi wao walipofanya upekuzi nyumbani kwake, waligundua vyeti nyake vya elimu havikuwapo. "Ni kweli tunaendelea na uchunguzi lakini kikubwa kama kuna mwenye taarifa zake ni ruksa kupokea lakini mpaka sasa bado hatujabaini yuko wapi.

"Kwa hali ilivyo mazingira yake bado hatujampata kwa sababu aliondoka na simu zake na vyeti vyake, hatujawahi kupata taarifa zake kwamba alipata kazi sehemu nyingine, kama tungepata simu yake inasomeka wapi ingekuwa ni rahisi kusema chochote, kwasababu wakati wa ukaguzi tulikuta vyeti vyake havipo," alisema.

Masunga alikuwa muuguzi wa idara ya masikio, pua na koo (ENT).

Inaelezwa kuwa Masunga alitoweka katika mazingira ya kutatanisha Julai 2, mwaka huu, nyumbani kwake, Mtaa wa Rau Pangaleni, Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro alikokuwa akiishi.

Wakati Masunga anatoweka alikuwa mapumziko ya siku mbili, kati ya Julai 2 na 3, mwaka huu.



Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Japhari Kubecha, akizungumza na waandishi wa habari wilayani humo juzi, wakati akitoa wito kwa wananchi kujitokeza kwa wingi kushiriki katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya kuchagua viongozi wenye maslahi mapana kwa Taifa. **PICHA: ASHRACK MIRAJI**

# Hemed ataka ukaguzi kuendana na teknolojia

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka wakaguzi wa ndani nchini kuendena na mabadiliko ya kukua kwa teknolojia ikiwa ni pamoja na kutumia changamoto za kiuchumi katika mataifa ya Afrika kuwa fursa ili kufikia malengo kwa pamoja.

Akizungumza kwa niaba ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, makamu huyo alisema kuna haja kwa wakaguzi wa ndani kuendena na mabadiliko ya ukuaji wa teknolojia ili kuongeza tija katika utekelezaji wa majukumu ya wataalamu wa kada hiyo.

"Serikali itaendelea kushirikiana na wakaguzi wa ndani ili kuendelea kuimarisha shughuli za maendeleo ya wananchi na Taifa kupitia kazi za wakaguzi, kubwa zaidi ni kuendelea kuwa wabunifu na uwajibikaji katika kazi hiyo.

Hemed alitumia jukwaa hilo kueleza kuwa kada ya ukaguzi wa ndani ni msingi katika kuongeza tija na chachu ya maendeleo katika taasisi za umma na binafsi kwa kuzingatia maadili na miiko ya kazi, hivyo kuondokana na dhana ya kukinzana na serikali licha ya kuwa imekuwa msaada mkubwa katika kuibua mambo mbalimbali yanayo kinzana na maendeleo ya taasisi na taifa kwa ujumla.

Rais wa Taasisi ya Wakaguzi wa Ndani Tanzania (IIA), CPA Dk. Zelia Njeza, alisema kwa muda mrefu kada hiyo imekuwa ikikabiliwa na changamoto kadhaa ikiwamo kupatikana kwa Sheria ya Wakaguzi wa Ndani na muundo utakaosaidia kufikisha ajenda na mawazo yatolewayo na kazi ya wakaguzi katika taasisi zao.

"Kiu yetu kubwa ni kuona serikali inafanyia kazi ombi letu la kuwepo kwa Sheria ya Ukaguzi wa Ndani na tunashukuru mchakato wa kufanikisha hilo umeshaanza, hivyo tunaomba kufanyiwa kazi kwa haraka na kukamilika ili kuendena na kasi ya mabadiliko ambayo tunayaongelea katika mkutano huu wa 17 wa mwaka.

"Lakini pia tunaomba miundo ya wakaguzi wa ndani pia iangaliwe maana asilimia kubwa bado hawako vizuri kwenye miundo yao.

"Mkaguzi wa ndani anatakiwa kuripoti kwa mkuu wa taasisi, utawala na wakati mwingine kwenye bodi ya uongozi, hivyo tunaomba miundo hiyo pia iangaliwe ili kuongeza tija itokanayo na kazi ya ukaguzi wa ndani nchini," alisema.

CPA Benjamin Mashauri, Mkaguzi Mkuu wa Ndani Tanzania Bara, alisema wakaguzi wa ndani kutoka Tanzania bara na visiwani pamoja na mataifa mengine ya Afrika, alisema kuna changamoto muhimu ambazo zikifanyiwa kazi, kada hiyo itaendelea kuthaminika na kuona mchango wake.

Miongoni mwa changamoto hizo ni pamoja na kuwepo kwa viongozi wa taasisi kujichukulia uamuzi pasi na kufuata taratibu za kisheria suala ambalo linaondoa hadhi kada hiyo katika mazingira ya utawala bora.

# Halmashauri zaagizwa kutenga bajeti maalum elimu watu wazima

**Na Hamida Kamchalla,** HANDENI

HALMASHAURI za Mkoa wa Tanga zimetakiwa kuweka bajeti mahususi kwa ajili ya kuwezesha utekelezaji wa utoaji wa elimu ya watu wazima ili kuondoka changamoto zilizopo katika utoaji wa elimu hiyo.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Saitori Steven, alisema hayo jana kwenye kilele cha maadhimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo rasmi yaliyofanyika kimkoa wilayani Handeni.

Alisema elimu ya watu wazima ina mchango mkubwa katika kujenga ustahamilivu na ubunifu katika kuleta mabadiliko chanya, lakini pia kupambana na mmomonyoko wa maadili kwa jamii.

"Nitoe maelekezo kwa wakurugenzi wa halmashauri zote kutenga bajeti mahususi kutekeleza shughuli za elimu hiyo pamoja na elimu nje ya mfumo rasmi na kuanzisha vituo vya mfano vya programu za MKEJA na MEMKWA," alisema.

Pia aliwataka wakurugenzi kuzitambua takwimu za sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 na kudahili wote ambao hawajui kusoma, kuandika na kuhesabu ili kuanzisha vituo vya utoaji elimu kupitia programu hizo.

Ofisa Elimu ya Watu Wazima Mkoa wa Tanga, Joseph Shayo, alisema utoaji wa elimu ya watu wazima unakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwamo bajeti ndogo ya utekelezaji wa shughuli za elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi.

Alisema mkoa unaendelea kuhamasisha wadau mbalimbali kuwekeza katika programu za elimu hiyo kwa kushirikiana na halmashauri ili kuondoa tatizo la bajeti huku ukiendelea kuhamasisha wananchi wote wajitokeze kujiunga na kujiendeleza kupitia programu za MEMKWA, MUKEJA, elimu ya sekondari kwa njia mbadala pamoja na vyuo vya ufundi.

Shayo alibainisha kwamba kiwango cha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu kwa kundi la watu wenye umri wa miaka 15 na kuendelea ni asilimia 83 kulinganisha na asilimia 79.8 kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012.

"Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi mwaka 2022, wanaume wanaongoza kwa asilimia 87.7 ukilinganisha na wanawake ambao ni asilimia 78.8," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni, Mussa Mwanyumbu, aliwataka watu wazima ambao bado hawajapata elimu waende darasani kwani itasaidia pia katika kusimamia elimu ya watoto wao.

## TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Hadija Kopa, Nasma walivyotikisa, 'Mambo Iko Huku', 'Mtu Mzima Hovyo', enzi hizo

**Na Adam Fungamwango**





ILIKUWA ni patashika nguo kuchanika kwenye kumbi mbalimbali za burudani mwanzoni mwa miaka ya 2000 hadi katikati pale makundi mawili hasimu wakati huo Tanzania One Theatre (TOT) na Muungano Calture Troupe yalipokuwa wakiamua kushindana.

Makundi hayo ambayo yalikuwa na idara tofauti ndani ya kundi moja kama vile ngoma za asili, vichekesho, maigizo, sarakasi, taarabu na hata muziki wa dansi zilikuwa zikiweka mipambano yao ambayo yalikuwa yakivutia mashabiki wengi wakati huo, na wakiwa wamegawanyika pande mbili mithili ya mashabiki wa Simba na Yanga.

Na hasa kilichowagawanyisha zaidi ni muziki wa taarabu ambao wakati huo ulikuwa kwenye kilele cha mafanikio.

Kumbi zilifurika mashabiki kibao kwenda kushuhudia pambano kati ya TOT iliyokuwa ikiongozwa na John Komba upande mmoja na Nolbert Chenga upande wa Muungano ambapo kundi hili lilikuwa na kitu cha ziada ambacho baadhi ya makundi yalikuwa hayana, nacho ni maonyesho ya nyoka, hasa aina ya chatu.

Tukirudi kwenye taarabu ambayo ndiyo iliyoyafanya makundi haya kuwa maarufu zaidi, Khadija Kopa akiwa upande wa TOT na Nasma yeye alikuwa upande wa Muungano.

Kwa hali ya kawaida hata mashindano yao kwenye kumbi mshindi alikuwa hapatikani. Ni kwamba mashabiki wanakuwa wamegawanyika nusu kwa nusu. Kikubwa kilichokuwa kinafanyika pale ni biashara kwani walikuwa wanakusanya mashabiki wengi mno. Ilikuwa ni biashara kubwa ya muziki wa taarabu ambayo haijawahi kufanyika nchini.

Huku mtaani watu pia kulikuwa na mabishano kuwa nani zaidi kati ya TOT na Muungano. Ni kama Simba na Yanga tu, mshindi huwa hapatikani kwa kubishana.

Kwenye redio, hasa Redio One na kipindi chake cha 'Nani Zaidi' walikuwa wakiwapambanisha na kusababisha mchuano mkali wa simu zinazomiminika, ambapo mara kwa mara mshindi alikuwa hazidi kura tano kila upande.

Khadija Malkia wa Mipasho, pamoja na Nasma Hamisi 'Kidogo' waliyapamba makundi haya kwa nyimbo mbalimbali ambazo ziliufanya muziki wa taarabu kuwa tishio kwa aina zote za muziki zilizokuwapo nchini.

Kuna wakati taarabu ikachomoza kuwa ni aina ya muziki pendwa zaidi nchini na kutengezwa vipindi mbalimbali vya muziki huo tu.

Kabla ya nyimbo zao za kuzodoana na vijembe ambavyo ilikuwa si kwa uhasama zaidi ya ushindani ya kibiashara, waimbaji hao tayari walishakuwa maarufu kutokana na nyimbo mbalimbali ambazo walizitoa.

Kasheshe ilikuja pia pale Kopa alipoondoka kwenda nchini Oman baada ya kupata mkataba ambapo inasemekena walianzisha kundi lao la taarabu, lakini aliporudi nchini uongozi wa TOT ukakataa kumpokea. Akajiunga na Muungano ambako alimkuta hasimu wake Nasma.

TOT nao kuona hivyo, wakaona isiwe tabu, wakatumia nguvu kubwa kumchomoa Nasma kutoka Muungano naye akajiunga na TOT. Hii iliwachanganya mno mashabiki wa taarabu. Kwa sababu kulikuwa na mashabiki wa bendi, halafu kukawa na mashabiki wa Hadija na Nasma. Ikawagawanya tena. Ikarudisha upya upinzani wa waimbaji wao na makundi yao na maonyesho ya pamoja kwa ajili ya kupambana yakazidi kuchukua chati. Baadaye sana, Hadija alirejea TOT.

Twende sasa kwenye nyimbo ambazo ziliwafanya kuwa juu kama mgomba wa ndizi na kuchukuliwa kuwa ndiyo moja kati ya waimbaji taarabu wachache nchi hii walikuwa maarufu zaidi.

Khadija aliibuka na kibao matata 'Mambo Iko Huku' ambacho kilizua misamiati, misemo ya mizaha mitaani na kila kitu.

"Umekwisha umepwaya hoi waranda na njia, umebaki sura mbaya, mkogoro utakuua. Akutane nani wewe, akusifu nani wewe, ondoka kisirani wewe.

Je, taarabu ipo hapo, taarabu imo humo? Aipate wapi? Huyo kibuzi marika mtazame anavyojitikisa, sijali lolote, wewe, mambo iko huku.

Na kwenye mambo humo. Katika wenye taarabu humo, umebaki mchomo hata nywele huna, wingi wa kikomo. Waenda saluni si saizi yako, waachie wenye fani bibi, hasara kwako, nywele za kilioni ndiyo saizi yako." Ni baadhi ya mashairi yaliyomo kwenye wimbo huo wa TOT.

Nasma naye, akiwa na Muungano akatoka na kibao alichokiita 'Mtu Mzima Hovyo'.

Achia ngazi bibi mchuma unaondoka huo. Umepwelea naondoka naye, umeishiwa ninadunda naye, kipi cha kung'ang'ania, hakutaki hebu timua. Mtu ovyo unajihashua, unajisumbua.

Si zaizi yako wewe, unajilengesha hakutaki, kaona mambo iko huku taarabu imo, kaona mambo iko huku, we, utaumiza roho yako. Naringa huto mchukua mambo yangu yameshamzingua, kaona mambo yako huku taarabu imo we, utaumiza roho yako." Huyo ndiye Nasma.

Khadija naye akaja tena na 'Mtie Kamba Mumeo. "Kama unaweza mtie kamba mumeo umzuie, ukitahamaki chini kachimba mumeo ninae mie. Ninae mie natamba naye.

Mbio kanikimbilia, akaniomba mapenzi, nami nikamringia, kanizingua kichizi, nami nikamridhia, kila kitu la azizi.

Nikamwambia chukua upendacho la azizi."

Nasma ambaye alifariki dunia mwaka 2009, akaja na wimbo wenye mashairi haya.

"Bure utajikondesha na kujipa taharuki, eti wajifaharisha, yeye unammikili, mimi nakufahamisha, mahabuba hakutaki,

Kichekesho wachekesha masikini hujijui, kwake wajitamanisha, hakutaki koroboi."

Mambo yaliendelea hivyo, hadi walipomalizia na nyimbo kadhaa zikiwemo 'Niliwaze' 'Sanamu na Michelini' na kadhalika.

**Tuma meseji 0716 3505**









HABARI KIMATAIFA

# Kim atishia kuishambulia Korea Kusini kwa nyuklia

**PYONGYANG, Korea Kaskazii**

KIONGOZI wa Korea Kaskazini, Kim Jong Un ametishia kutumia silaha za nyuklia na kuisambaratisha kabisa Korea Kusini iwapo nchi hiyo itamchokoza.

Hayo ni kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na vyombo vya habari nchini humo. Na kwamba hiyo ni baada ya kiongozi wa Korea Kusini kuuonya utawala wa Kim kwamba utaangushwa iwapo atathubutu kutumia zana za nyuklia.

Ilielezwa kuwa Kim alitoa kauli hiyo wakati alipofanya ziara katika kitengo cha operesheni maalum cha jeshi.

"Iwapo Korea Kusini itajaribu kutumia jeshi kuingilia uhuru wa Korea Kaskazini, hali kama hiyo ikitokea, Seoul na Jamhuri ya Korea zitaangamia," alisema Kim.

Ilielezwa kuwa taarifa ya Kim ni jawabu kwa hotuba ya Rais wa Korea Kusini Yoon Suk Yeol, katika siku ya jeshi la taifa lake.

Majibizano kama hayo baina ya mataifa hayo mawili si jambo geni ila yanafanyika wakati ambako kuna uhasama mkubwa baina ya mataifa hayo kutokana na hatua ya Korea Kaskazini hivi majuzi kufichua kwamba ina kinu cha nyuklia na hatua yake ya kuendelea kufanyia majaribio makombora.

Wachambuzi walisema wiki ijayo, bunge la Korea Kaskazini linatarajiwa kupitisha na kutangaza rasmi uhasama baina ya mataifa hayo mawili katika Rasi ya Korea, hatua itakayokuwa kiashiria rasmi cha kukataa maridhiano na Korea Kusini na kuweka mipaka mipya ya mataifa hayo.

Tangu mwaka 2022, Kim mara kwa mara amekuwa akitishia kutumia silaha za nyuklia ila wachambuzi wanasema hakuna uwezekano wake wa kutumia silaha hizo kwa kuwa jeshi la Korea Kaskazini ni dogo likilinganishwa na jeshi la Marekani na wandani wake.

Julai, mwaka huu, Korea Kusini na Marekani zilisaini mwongozo wa ulinzi utakaozijumuisha silaha za Korea Kusini na zile za nyuklia za Marekani, kwa ajili ya kukabiliana vyema na Korea Kaskazini na mpango wake wa nyuklia unaozidi kuimarika. Licha ya Korea Kusini kutokuwa na zana za nyuklia.

Uhasama baina ya mataifa hayo ya Korea uko katika kiwango kibaya zaidi kuwahi kushuhudiwa katika kipindi cha miaka kadhaa, huku uchokozi wa Kim wa majaribio ya makombora na mazoezi ya kijeshi ya Korea Kusini kwa ushirikiano na Marekani, vikionekana kama vitendo vya kulipiziana kisasi.

Pia ilielezwa kuwa kuna mawasiliano kati ya Korea hizo mbili tangu mwaka 2019.

Jeshi la Korea Kusini lilisema kwamba Korea Kaskazini imeanza tena kurusha maputo yaliyobeba taka kuelekea nchini humo. Ilielezwa kuwa Pyongyang ilikuwa ikirusha maelfu ya maputo hayo tangu mwishoni mwa mwezi Mei jambo lililoipelekea Korea Kusini kuanza tena kutangaza propaganda dhidi ya utawala wa Korea Kaskazini katika maeneo ya mpakani.

*APE, DW*

# Waliokufa ajali ya boti Congo wafikia 78

**KINSHASA, DRC**

IDADI ya watu waliofariki kutokana na mkasa wa kuzama kwa boti nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) imefikia 78 huku juhudi za kuwatafuta wengine zikiendelea siku moja tangu mkasa huo ulipotokea.

Gavana wa Mkoa wa Kivu Kusini, Jean Jacques Purusi, alisema jana kuwa idadi hiyo ya vifo ni ya awali na kuna uwezekano mkubwa ikaongezeka wakati waokoaji wanajaribu kuwatafuta wengine ambao bado hawajulikani walipo.

Alisema taarifa zinaonesha chombo hicho kilichozama kwenye Ziwa Kivu kilikuwa kimepakia abiria wasiopungua 278 kilipong´oa nanga kutoka bandari ya Minova iliyopo Kivu Kusini kuelekea mji wa Goma uliopo kwenye mkoa jirani wa Kivu Kaskazini.

Mashuhuda wanasema boti hiyo ilizima mita chache kutoka Bandari ya Kituku ilipokuwa inajaribu kutia nanga na saa kadhaa baadaye waokoaji waliopoa miili ya watu 50.

Ilielezwa kuwa hadi sasa maofisa wa msalaba mwekundu wanaendelea na shughuli za uokoaji kutafuta miili iliyozama.

*DW*



Wahudumu wa afya wakihudumia majeruhi katika eneo la ajali Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) jana. **PICHA: MTANDAO**

# Viongozi Afrika kushiriki mkutano wa Francophonie

**PARIS, Ufaransa**

WAKUU kadhaa wa nchi na serikali kutoka nchi wanachama wa Shirika la Kimataifa la Francophonie (OIF) watakutana nchini Ufaransa kuzungumza juu ya mustakabali wa lugha ya Kifaransa na migogoro mikubwa ya kimataifa ya sasa.

Inaelezwa kuwa hafla hiyo itakayodumu kwa siku mbili ambayo Ufaransa haijaandaa kwa miaka 33 itahudhuriwa pia na viongozi wengi wa Afrika.

OIF yenye wanachama 88 ambao wamejiwekea nia ya pamoja ya kukuza lugha ya Kifaransa kote ulimwenguni, ikielezwa kuwa kwa sasa inazungumzwa na watu milioni 320 duniani.

Ilielezwa kuwa OIF itampokea rasmi katika hafla hiyo mwanachama mpya, ambae ni Ghana, wakati Angola itajiunga rasmi na shirika hilo kwa hadhi ya mwangalizi.

Viongozi wote ambao wamethibitisha ushiriki wao watakutana kwa mara ya kwanza kaskazini mwa Ufaransa, ambako kwa siku ya kwanza wataangazia suala la kidijitali na utamaduni kwa mada ya mwaka huu.

Kama sehemu ya mlolongo wa kisiasa wakuu wa nchi na serikali watakutana kwa faragha karibu na Rais Macron kujadili migogoro mikubwa ya kimataifa ya sasa, ikiwamo ya Mashariki ya Kati ambako Lebanoni yenyewe ni mwanachama OIF.

Inaelezwa kuwa Lebanon inakabiliwa na mashambulio ya Israel na kwamba kuongezeka uhasama kati ya serikali ya Kiyahudi na Iran kunazua hofu ya kusambaa kwa mgogoro katika eneo ukanda wote.

Ilielezwa kuwa kutokuwapo kwa mataifa ya Sahel na hali ya mashariki mwa Kongo DRC ni miongoni mwa masuala yatakayojadiliwa.

Wakati huo huo, ilielezwa kuwa mijadala hiyo pia inapaswa kulenga masuala kadhaa ya Kiafrika.

*RFI*

# Ujenzi kituo cha polisi kusogeza huduma, kukabiliana na uhalifu

**Na Maulid Mmbaga**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mhandisi Hamad Masauni, amesema kukamilika kwa ujenzi wa kituo cha polisi cha Daraja B Wilaya ya Chemba, mkoani Dodoma kunakwenda kusogeza huduma za kipolisi karibu na wananchi.

Masauni aliyasema hayo jana wilayani Chemba wakati akiweka jiwe la msingi la ujenzi wa kituo hicho cha polisi ambacho unagharimu Sh. milioni 350 na mpaka upo katika hatua za mwisho.

Alisema dhamira ya serikali ni kulisogeza Jeshi la Polisi karibu zaidi na wananchi kupitia sera ya Polisi Jamii na ndio maana kuna askari wa cheo cha nyota moja katika kata zote nchi nzima.

"Serikali inafanya maboresho ya mazingira ya kufanyia kazi askari wa Jeshi la Polisi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vipya na vya kisasa na vitendea kazi stahiki kwa askari," alisema.

Masauni alisisitiza Jeshi la Polisi kuendana na maboresho hayo yanayofanywa na serikali kwa utendaji kazi mzuri unaozingatia weledi na maadili ya kazi zao ili kuakisi jitihada za serikali katika kutatua kero za wananchi.

Akiwa Kata ya Pahi, Wilaya ya Kondoa, katika mkutano wa hadhara alifanya harambee ya kuchangia ujenzi wa kituo cha polisi kata na kupata Sh. milioni 18.4 ambazo zitawezesha ujenzi kuanza mwezi ujaa.

Waziri Masauni ambaye yuko katika ziara ya kikazi mkoani Dodoma, pia ametembelea na kuunga mkono jitihada za wananchi katika ujenzi wa Shule ya Sekondari Mnenia, Kondoa na kukagua na kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Bolisa, Halmashauri ya Kondoa Mjini.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene (kulia), akifurahia jambo na wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kutwa Ingri, baada ya kuwasili katika Halmashauri ya Wilaya ya Rorya, kwa ajili ya kuzindua shule hiyo wakati wa ziara yake ya kikazi mkoani Mara juzi. **PICHA: UTUMISHI**

# Waziri asisitiza usimamizi miradi kwa usahihi

**Na Mwandishi Wetu, SERENGETI**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, amewataka viongozi wa Mkoa wa Mara kutekeleza miradi ya maendeleo kwa usahihi ili idumu kwa muda mrefu na kutumika kikamilifu na wananchi.

Akizindua ujenzi wa zahanati ya Getarungu uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani kupitia Shirika ya Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) juzi, wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kusikiliza changamoto za wananchi katika Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti mkoani Mara, Simbachawene alisema ameridhishwa na utekelezaji wa mradi wa zahanati hiyo na kutaka halmashauri za mkoa huo kuiga utekelezaji wa namna hiyo.

"Nimefurahi sana kupitia ziara hii nzuri, kubwa nililojifunza ni utekelezaji wa miradi kwa usahihi sana. Tujifunze na sisi halmashauri kuangalia miradi inayotekelezwa kwa usimamizi mzuri inavyokuwa na je, sisi tunashindwa wapi? alisema.

Alisema mradi huo umesimamiwa na mkandarasi maalum na umekuwa wa kuridhisha sana lakini kwenye halmashauri ambako makandarasi wanalipwa mishahara, miradi yao inakuwa si ya kuridhisha.

"Nimezindua zahanati hii ya Getarungu kwa kujidai sana, ni nzuri inafurahisha. Nawasisitiza viongozi katika halmashauri kuiga mfano huu mzuri. Tukiendelea kutosimamia kwa usahihi tutachukuliana hatua," alisisitiza.

Simbachawene alisema utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo ni maono ya Rais Samia Suluhu Hassan ambaye amefanya jitihada za kukuza utalii, kuongeza pato la taifa kupitia sekta ya utalii na kujenga uhusiano mzuri na wadau wa maendeleo na ndiyo sababu ya kupatikana kwa mradi wa zahanati nane kwa mara moja katika wilaya ya Serengeti ikiwamo ya Getarungu.

Simbachawene ameendelea na ziara ya kikazi ya kukagua utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo na kuzungumza na wananchi katika mkoa wa Mara.

# Makada wawili CHADEMA watimkia ACT-Wazalendo

**Na Gideon Mwakanosya, SONGEA**

MAKADA wawili wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mkoani Ruvuma akiwamo aliyewahi kuwa Mwenyekiti wa chama hicho katika mkoa huo, Josephu Fuime, wametangaza kuhamia Chama cha ACT Wazalendo.

Mwingine ni Edmund Nditi, aliyewahi kuwa diwani wa Luanda (CHADEMA) Jimbo la Mbinga Vijijini (2015-2020).

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Fuime alitaja sababu za kuhama ni uroho wa madaraka viongozi wa ngazi ya juu CHADEMA.

Alisema amehama baada ya kuona CHADEMA kuna mazingira yaliyozungukwa na harufu ya siasa ambayo inaonesha kuwa hakuna demokrasia ya kweli zaidi ya kusemwa mdomoni.

Fuime alisema mwaka 2004 alijiunga na CHADEMA na baadaye kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa chama hicho Mkoa wa Ruvuma, akihudumu kwa miaka 10 (2009-2014).

Alisema amewahi kuwa diwani wa Kata ya Mjini Manispaa ya Songea Mjini na mwaka 2015 CHADEMA kilimpitisha kugombea ubunge Jimbo la Songea Mjini na kumwagwa na mgombea wa CCM, Leonidas Gama, ambaye wakati huo alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro.

Nditi alisema ameamua kuondoka CHADEMA na kujiunga ACT Wazalendo kwa sababu wamekuwa wakipigania haki ya jamii.

Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Doroth Semu, alisema kuwa wanaendelea kupigania haki za Watanzania.

**Alisema amehama baada ya kuona CHADEMA kuna mazingira yaliyozungukwa na harufu ya siasa ambayo inaonesha kuwa hakuna demokrasia ya kweli zaidi ya kusemwa mdomoni.**

# HADITHI

TAARIFA za habari kwenye televisheni, redio, mitandao ya kijamii zinaarifu kutekwa kwa mtoto wa miaka sita, Macaire, mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja Mbezi Dar es Salaam. Mashuhuda wanasema alinyakuliwa na mwanaume mmoja aliyeshiba, kujaa misuli na kukimbilia kwenye gari lililokuwa pembeni mwa barabara ya Bagamoyo ambalo mlango wake ulikuwa wazi. Wazazi wa mtoto wanapigiwa simu na watekaji wakitaka kiasi cha Sh. Milioni 15 ili wamwachie. Jeshi la Polisi linaingia kazini kumsaka au kuwasaka watekaji. Walichogundua ni kisa cha kushangaza, kusisimua ambacho utakipata utakaposoma kila aina ya nakala ya gazeti hili ili kuupata mkasa mzima wa tukio.

# Damu ya Mariamu-33

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri.

Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging.

Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile.

Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani.

Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

***************************************

Kamal alitambua kuwa anatafutwa na pande mbili. Tayari Jeshi la Polisi limeaminishwa kuwa yeye ni muuaji, hivyo linamsaka ili limpeleke mahakamani, lakini watesi wake waliomsingizia kesi bado wanaona wanaweza kuchomoka hivyo ili kufunga mjadala ni kumfanya anyamaze, asiongeaa milele.


Alipohakikisha amepata kila alichokihitaji alifunga droo zote kama vile hazikufunguliwa. Akatoka nje. Akamkuta afande Willy akiwa ameimarisha ulinzi wa ndani na nje. "Vipi huko?" "Yaani huku kila kitu nimemaliza, nimepata kila aina ya ushahidi." Wakagongeana mikono. Afande Willy, akaenda kuziweka silaha za askari wale waliokuwa bado hawajazinduka sehemu ya uficho kidogo ili zisionwe na kila mtu. Badala yake wataziona wakianza kuzitafuta. Kamal alikuwa amebeba mkoba, huku Afande Willy akiwa amebeba mfuko ambao una matambara ambayo rafiki yake alikuwa akiyavaa kwa kujifanya mwendawazimu.

Waliondoka wakiwa washindi hadi mbele ya kituo cha Makumbusho walipokuwa wakiacha gari walilopewa na dokta Shija, wakarejea maskani kwenda kupanga plani nyingine ambayo itaendeleza kile walichokusudia.

Kazi iliyobaki ni kuanza kuujulisha umma nani alihusika kwenye mauaji ya msichama mrembo Mariamu.

Hiki ndicho hasa kilikuwa kinamtisha Materu. Alijua wakati wowote kinaweza kunuka. Waliovamia jengo hilo na kuwapiga walinzi bila kuchukua chochote zaidi ya flashi hizo tu hawakuwa watu wa kawaida.

Hakuwa mjinga kudhani wamezichukua kwenda kuzitunza nyumbani kwao, bali ni kuzitoa mbele za wananchi ili kujua nini kiliendelea. Kichwa kilimuuma.




**Kilichokuja kubainika ni kwamba tayari Materu na wapambe wake walikuwa wameshapita kwenye vyombo vingi vya habari na kujaribu kuzuia habari yoyote itakayomhusu.**

************************************

Walikaa kwenye kochi na kucheka sana. Tayari walikuwa wamekamilisha asilimia 80 ya kazi yote. Kazi iliyobaki ni kuuonyesha ulimwengu Boniphace Materu ni mtu wa aina gani. Nje anaonekana ni mtu safi, mwenye busara na huruma mbele za watu. Ni mtu anayependwa na kuheshimiwa sana. Lakini ndani ni mtu mbaya, katili, muuaji, asiye na hata chembe ya huruma.

Kamal alionekana kuwa ni mtaalam kidogo wa mambo ya teknolojia kuliko afande Willy, aliiweka kompyuta mpakato yake mezani. Akatoa flashi zote mbili na kubwaga mezani. Akaanza akachomeka moja. Akawasha na wakaanza kuangalia kile ambacho kiliwafanya wazisake kwa udi na uvumba flashi hizo.

Walipomaliza ya kwanza ambayo haikuwa na chembe ya shaka kuwa itaifanya nchi kutikisika, wakaweka nyingine. Walipomaliza zote wakaridhika. Sasa kilichobaki ni kumwaibisha Materu, ambaye tayari pia ameshaanza kuonyesha nia ya kugombea ubunge kwenye moja ya jimbo la mkoa wa Kilimanjaro.

Ilikuwa kama bahati nzuri tu. Afande Materu alikutana na mtu ambaye alikuwa anafanya kazi kwenye jengo ambalo ndiyo ofisi za Materu ziliko.

Wakati wanaongea, akadokezwa na mtu huyo kuwa jamaa hakuwa mtu mzuri, ana mambo mengi mabaya ambayo watu wengi hawayajui.

Wakati wakiongea hayo, jamaa huyo alikuwa hajui kwamba Willy ni askari. Akamwambia yeye alikuwa anafanya kazi hapo na anajua mambo yake mengi na anafahamu hata vikao vyake vya siri alivyokuwa akikaa na wenzake kwa ajili mipango haramu ambayo yeye alikuwa haifahamu vyema.

Akamhabarisha kuwa huwa wanarekodi mazungumzo yao na flashi zao wanazifungua kwenye droo zilizopo ofisini hapo.

Mazungumzo hayo yalimfurahisha afande Willy, kwani alijua anayezungumza hapo ni yule mtu wanayemhitaji sana na kupata ushahidi.

Baada ya kugundua kuwa mtu yule alifukuzwa kazi kutokana na utovu wa nidhamu, anaweza kuwa msaada mkubwa kwake kwani ana hasira.

Tamim, ndiye aliyemhabarisha afande Willy, ramani ya jengo lote la Makumbusho, zilipo ofisi za Materu, droo anazohifadhia flashi na nyaraka zake muhimu.

Willy aliamua kumpeleka kwa kaka yake dokta Shija ambaye alimlipa fedha kwa ajili ya uwezekano wa kupata funguo za mlango mkuu wa jengo, ofisi za Materu na droo zake.

Haikuwa kazi kubwa kwa Tamim, kwani alishawahi kufanya kazi hapo, na alikuwa na marafiki zake, hivyo alichofanya ni kama anakwenda kuwasalimia.

Alikuwa na kipande cha sabuni, na akatumia wenyeji wake kupata funguo hizo na kuzikandamiza kwenye sabuni, na kubakisha chapa yake.

Aliondoka hapo akiwa na chapa za funguo tatu, ambazo alizipeleka kwa afande Willy, naye alimkabidhi mtaalam ambaye kwa kutumia chapa hizo, alichonga funguo bandia ambazo ndizo Kamal alizitumia kufunga milango yote pamoja na droo.

Kazi iliyofuata ni kuanza kufanya uchunguzi ni, magazeti, redio na televisheni gani zinaweza kutumika kuanzisha sakata hilo.

Kilichokuja kubainika ni kwamba tayari Materu na wapambe wake walikuwa wameshapita kwenye vyombo vingi vya habari na kujaribu kuzuia habari yoyote itakayomhusu.

Ilifanikiwa kwa kiasi fulani, lakini baadhi ya waandishi za uchunguzi walipata fununu ya hilo na wakaingia chimbo kuisaka habari hiyo.

Waandishi watatu wa magazeti walikutana na Kamal eneo la siri ambalo hata wao hawakujua ni wapi, wakamhoji kuhusu kuhusika kwake kwa mauaji ya mpenzi wake, ndipo alipowahadhithia kila kitu ikiwamo ushahidi unaoonyesha kuwa bosi wake, Materu ndiye aliyehusika kwa mauaji hayo.

Akawapa ushahidi wa maandishi na video ili hata kama akishtaki, basi ajikaange mwenyewe kwenye mafuta yake.

Siku tatu baadaye, kwa msaada wa dokta Shija, waandishi wengine wa habari za mitandao ya kijamii walipelekwa eneo lingine kwa ajili ya mahojiano.

Nao waliambiwa kila kitu, na kupewa ushahidi, ambao wanahabari zote walikuwa wakipewa kopi, hata flashi nazo zikikopiwa na kupestiwa, ili mwenyewe abaki na ushahidi halisi ambao ungeweza kumsaidia kuepuka kesi inayomkabili.

Baada ya kukamilisha zoezi hilo, ahadi ya kulipua bomu ilikuwa ni Jumatatu. Ndiyo siku ya kwanza ya juma. Ndiyo siku ambayo watu wanakuwa na nguvu za kufanya kazi baada ya mapumziko ya wiki.

Wote waliona siku hiyo ndiyo inafaa, hivyo wakaacha kwanza watu wale wikiendi, na Jumatatu wapate kitu cha kushtua. Kitu ambacho kitabadilisha kila kitu. Kitabadilisha mtazamo wa raia na askari polisi juu ya mauaji ya mrembo Mariamu.

***Itaendelea Jumamosi***

## Kipa Dodoma Jiji FC afanya makubwa

**Na Adam Fungamwango**

MLINDA mlango wa Dodoma Jiji, Alain Ngeleka, juzi alikuwa kipa wa kwanza msimu huu kutoa pasi ya bao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiisaidia timu yake kushinda mabao 2-0 dhidi ya Tabora United.

Katika mchezo huo uliopigwa kwenye Uwanja wa Jamhuri Dodoma, Ngeleka aliupiga mpira mrefu dakika za majeruhi wakati timu yake ikiongoza bao 1-0, ulikwenda moja kwa moja hadi kwenye eneo la hatari la Tabora United, ukadunda na kuwapoteza maboya mabeki, kabla ya kumkuta Waziri Junior, ambaye aliwahadaa walinzi na kuukwamisha wavuni kwa mguu wa kushoto.

Si mara nyingi sana kwa makipa kutoa 'asisti' kwenye mchezo wa soka, lakini kipa huyo raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, aliyesajiliwa na Dodoma Jiji mwanzoni mwa msimu akitokea Kagera Sugar alifanya hivyo na kuingia kwenye rekodi ya soka nchini.

Katika mchezo huo wa raundi ya saba, bao lingine la Dodoma Jiji liliwekwa wavuni na Paul Peter.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mecky Maxime, amewapongeza wachezaji wake, akisema wamecheza mchezo mgumu katika mazingira magumu kwa sababu ni siku chache tu wametoka kucheza dhidi ya Simba, walifungwa bao 1-0 na Wekundu wa Msimbazi.

"Tulicheza mechi ngumu dhidi ya Simba na tukacheza mechi hii nyingine ngumu dhidi ya Tabora United, hatukufanya maandalizi sana kwa sababu hatukuwa na muda, ila niliwaambia tu wachezaji wangu kuwa kile mlichokifanya dhidi ya Simba, mkikiweka hapa tunashinda na kweli ikawa hivyo," alisema Maxime.

Naye Kocha Mkuu wa Tabora United, Francis Kimanzi, alilia na safu yale ya ulinzi, huku akiwapongeza wapinzani wao Dododa Jiji.

"Tunawapongeza wapinzani wetu, kwetu sisi inabidi tulifanyia kazi sehemu yetu ya ulinzi kwa sababu ilikuwa inafanya makosa mengi, najua tuna wakati mgumu lakini tunajitahidi katika michezo ijayo," alisema Mkenya huyo.

Matokeo hayo yanaifanya Dodoma Jiji kupaa hadi nafasi ya saba ikiwa na pointi tisa kwa michezo saba iliyocheza, Tabora United yenye pointi kama hizo ikifuatia, ikiwa pia imecheza mechi saba.

# KAGERA SUGAR YAFUNGUKA HAIFAHAMU INAPOKWAMIA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake kupoteza mechi tano za Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya michezo saba waliyocheza, Kocha Mkuu wa Kagera Sugar, Paul Nkata, amesema anashangazwa na hali hiyo huku akijiuliza tatizo hajui kama tatizo ni yeye au wachezaji wake.

Akizungumza baada ya mchezo wa raundi ya saba ya Ligi Kuu, ikichapwa bao 1-0 dhidi ya KMC, uliochezwa Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi, Nkata alisema haelewi kwa nini wanapata matokeo mabovu wakati anatoa mbinu zote za ufundi kwa wachezaji wake.

"Kusema kweli nimetoa kila aina ya ufundi, lakini hali imekuwa hivi, sasa sijui kama sisi makocha si wazuri au au wachezaji, tumekuwa hatufanyi vizuri," alishangaa kocha huyo.

Mbali na hilo, Nkata alilalamikia baadhi ya maamuzi mabaya kwa marefa hasa timu yake inapocheza ugenini.

"Tumefungwa, lakini mechi nyingi tukicheza ugenini kunakuwa na tatizo la uchezeshaji usio wa haki, lakini ndiyo mpira," alisema kocha huyo raia huyo wa Uganda.

Kwa matokeo hayo, Kagera Sugar yenye pointi nne, ikishinda mechi moja na sare moja, iko katika nafasi ya 14 kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Naye Kocha Mkuu wa KMC, Abdulhamid Moallin, amewapongeza wachezaji wake kwa kushinda mchezo huo, akisema walicheza wakiwa wamechoka, lakini walijituma.

Moallin alisema mechi iliyopita dhidi ya Yanga iliwachosha wachezaji wake, lakini akashukuru kwa kupata ushindi huo baada ya kutoka kufungwa.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa nguvu walioonyesha, licha ya kuingia kwenye mchezo huu wakiwa wamechoka, tumecheza na timu ngumu, tulicheza vyema hasa kipindi cha kwanza na kukosa nafasi nyingi, tunashukuru kwa ushindi kwa sababu inatupa morali wa kufanya vyema mechi inayokuja baada ya mapumziko," alisema Moallin.

KMC sasa imefikisha pointi nane na kupaa hadi nafasi ya nane, ikiwa imeshuka dimbani mara saba.



Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiwalani, Dar es Salaam wakifanya mazoezi ya mchezo wa mpira wa magongo kwenye Uwanja wa JKM Park jijini juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga Princess yasaka rekodi

**Na Mwandishi Wetu**

TUNATAKA kuweka rekodi, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, kuelekea mechi ya fainali ya Ngao ya Jamii ya Wanawake dhidi ya JKT Queens itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Lema aliliambia gazeti hili hakuna kingine wanachotarajia zaidi ya kutwaa taji la Ngao ya Jamii kwa mara ya kwanza tangu lilipoanza kuchezwa msimu uliopita likichukuliwa na watani zao, Simba Queens.

"Tumejipanga mimi na wachezaji wangu, ushindi dhidi ya Simba Queens umewapa vijana wangu morali, na nguvu ya kuingia katika mchezo wa kesho (leo).

Tunajua JKT Queens siyo timu ya masihara, ni timu ngumu iliyokaa kwa muda mrefu lakini mimi wachezaji wangu wengi wapya, lakini tayari wameshaanza kujiamini, wanaweza kufanya kitu," alisema Lema.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Queens, Esther Chabruma, amesema wanakwenda kwenye fainali hiyo kucheza soka na hawataidharau hata kidogo, Yanga Princess.

Chabruma alisema aliona mchezo ambao timu hiyo imecheza dhidi ya Simba Queens na kugundua wamefanya usajili mzuri.

"Wamefanya usajili mzuri, kwa maana hiyo hatuendi kucheza kama tunacheza na Yanga Princess ili tunayoijua, imebadilika, lakini lengo letu na kuchukua ubingwa baada ya kuukosa msimu uliopita dhidi ya Simba Queens," alisema Chabruma.

Yanga Princess iliingia fainali kwa kuifunga Simba Queens penalti 4-3 baada ya kutoka sare ya bao 1-1, huku JKT Queens iliiadhibu Ceasiaa Queens mabao 7-0.

Fainali hiyo itatanguliwa na mchezo wa kusaka mshindi wa tatu kati ya Simba Queens dhidi ya Ceasiaa Queens kutoka Iringa.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SOUTHGATE KUTUA EVERTON

MMILIKI mtarajiwa wa Everton, Dan Friedkin, amemtambua kocha wa timu ya taifa ya England, Gareth Southgate, mwenye umri wa miaka 54, kama mtu anayetarajiwa kuchukua nafasi ya Mwingereza mwenzake, Sean Dyche (53), kwenye Uwanja wa Goodison Park. ***(GiveMeSport)***

### WIRTZ ATAJWA LIVERPOOL

LIVERPOOL inajiandaa kuivamia Bayer Leverkusen kwa kiungo wao wa Ujerumani, Florian Wirtz mwenye umri wa 21, mlinzi wa Uholanzi, Jeremie Frimpong (23), na kiungo wa kati wa Argentina Exequiel Palacios (25). ***(CaughtOffside)***

### ZUBIMENDI SOKONI EPL

LIVERPOOL pia wameonyesha nia ya kumsajili kiungo wa Hispania, Martin Zubimendi, mwenye umri wa miaka 25, kutoka Real Sociedad katika msimu wa Januari wa usajili wa wachezaji. ***(Fabrizio Romano)***

### GOMEZ AGEUKA LULU

MLINZI wa Liverpool na England, Joe Gomez, mwenye umri wa miaka 27, anawaniwa na klabu za Aston Villa na Newcastle United. ***(Football Insider)***

### MADRID, BARCELONA VITANI

REAL Madrid inamfuatilia mlinzi wa Nottingham Forest, Murillo, mwenye umri wa miaka 22, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka Barcelona na Bayern Munich ili kumpata Mbrazil huyo. ***(HITC)***

### GOMES AGOMBEWA ENGLAND

KLABU za Newcastle United, Manchester United na Tottenham Hotspur ni miongoni mwa klabu zinazovutiwa na kiungo wa kati wa Lille na England, Angel Gomes, mwenye umri wa miaka 24. ***(GiveMeSport)***

### BARCELONA YAHITAJI KIPA

BARCELONA itarajiwa kufanya mazungumzo ya dharura wiki hii ili kujadili iwapo watamleta golikipa mpya kuchukua nafasi ya mchezaji wao wa kimataifa wa Ujerumani aliyejeruhiwa, Marc-Andre ter Stegen. ***(ESPN)***

### DIAZ KUULA LIVERPOOL

LIVERPOOL inatarajiwa kufanya mazungumzo na winga wa Colombia, Luis Diaz, mwenye umri wa miaka 27, kuhusu mpango wa kuongeza mkataba wake hadi 2027 kufuatia mwanzo wake mzuri wa msimu huu. ***(Football Insider)***

### LARSSON NYOTA MPYA

KLABU kadhaa zinamfuatilia winga wa Eintracht Frankfurt aliye na umri wa miaka 20 kutoka Sweden, Hugo Larsson. ***(Fabrizio Romano)***

### SOUTHAMPTON, DIBLING KUTETA

KLABU ya Southampton inatumaini kumshawishi kiungo wa kati wa England, Tyler Dibling, mwenye umri wa miaka 18, kusaini mkataba mpya huku Manchester United wakionyesha nia ya kutaka kumnunua nyota huyo. ***(GiveMeSport)***

### CONNOLLY ANUKIA SUNDERLAND

KLABU ya Sunderland inatazamia kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Brighton na Jamhuri ya Ireland, Aaron Connolly mwenye umri wa miaka 24, kutoka Hull City. ***(Sun)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# TEN HAG: WACHEZAJI WANGU 'WALIZIMIKA'

## ●●● Hata hivyo amewasifu wachezaji kwa kupambana kusaka...

**PORTO, Ureno**

ERIK ten Hag aliwashutumu wachezaji wake „walizimika" wakati Manchester United ikitoka kuongoza mabao mawili na kuambulia sare ya magoli 3-3 dhidi ya FC Porto kwenye mchezo wa Ligi ya Europa uliochezwa juzi usiku.

United ilihitaji bao la dakika za lala salama kutoka kwa Harry Maguire, kama mchezaji wa akiba wa kipindi cha pili, ili kuokoa pointi moja huko Ureno.

Kikosi cha Ten Hag kilikuwa mbele kwa mabao 2-0 baada ya dakika 20 tu kwenye Uwanja wa Dragao, lakini wakaruhusu magoli mawili ndani ya dakika saba hadi walipokwenda mapumziko.

United walipata bao tena baada ya kipindi cha mapumziko na nahodha Bruno Fernandes kutolewa kwa kadi nyekundu kwa mchezo wa pili mfululizo kabla ya bao la dakika za lala salama la Maguire.

"Ni hisia mchanganyiko," alisema Ten Hag akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulifunga mabao mawili kisha tukazima. Hatuwezi kumiliki mpira na kulinda, tunazima. Tunaruhusu bao la kwanza bila ya lazima kabisa halafu unawasha moto kwenye uwanja huu na unakuwa mgumu sana.

"Lakini basi lazima niwasifu vijana, jinsi wanavyorejea kwenye mchezo na jinsi wanavyopambana na kutafuta njia ya kupata bao la kusawazisha."

Ten Hag pia alilazimika kutetea uamuzi wake wa kumtoa Marcus Rashford wakati wa mapumziko licha ya nyota huyo kufunga bao la kwanza la United lakini kwa kushangaza nafasi yake ilichukuliwa na Alejandro Garnacho wakati wa mapumziko.

Hapo awali Ten Hag alisema Rashford alibadilishwa ili kumfanya fowadi huyo kuwa fiti kabla ya safari ya kuelekea Aston Villa hapo kesho.

Lakini akizungumza katika mkutano wake na wanahabari, Mholanzi huyo alidokeza alifanya mabadiliko baada ya mabao yote mawili ya Porto ya kipindi cha kwanza kupitia krosi kutoka kwa upande wa Rashford.

„Garnacho alikuwa mchezaji wangu bora siku ya Jumapili kwa mbali na pia katika michezo mingine mingi," alisema Ten Hag alipoulizwa kwa nini Rashford alitolewa.

"Nadhani katika msimu huu ninavyoutathmini hadi sasa, anatuletea tishio la ushambuliaji kwa kutengeneza nafasi, pasi za mabao, pia kufunga. Garnacho pia tulilazimika kumchezesha na tuna wachezaji wawili wazuri zaidi ya hapo.



# RUDIGER ASHANGAA UBORA WA YAMAL

**MADRID, Hispania**

MLINZI wa Real Madrid, Antonio Rüdiger amesema "inatisha sana" jinsi mshambuliaji wa Barcelona, Lamine Yamal, alivyo bora akiwa na umri wa miaka 17 tu.

Yamal aliingia uwanjani kwa Barcelona akiwa na umri wa miaka 16 msimu uliopita lakini ni uchezaji wake kwenye Euro 2024 ambao ulishuhudia wasifu wake ukiongezeka, aliingia katika ushindi wa Hispania kwenye mashindano hayo na akachaguliwa kuwa Mchezaji Chipukizi wa Mashindano.

"Lazima utoe ukweli unapostahili," alisema Rudiger akiiambia podcast ya The Inside Scoop alipoulizwa kuhusu Yamal.

"Ana umri wa miaka 17 tu. Mchezaji ambaye tayari yuko Barca, akiwa na umri wa miaka 17, inatisha sana. Alichokifanya kwenye Euro, lazima umpe pongezi. Ana mustakabali mzuri mbeleni.

"Nadhani Barca wana mchezaji ambaye ana kazi kubwa na ninatumaini ataendelea kuwa na afya."

Yamal amefunga mabao manne na kutengeneza mengine matano katika mechi 10 za ligi kwa vinara hao wa LaLiga msimu huu.

# Adeyemi atajwa kumrithi Salah

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL wanamchunguza winga wa Borussia Dortmund, Karim Adeyemi na wako tayari kulipa hadi euro milioni 50 kwa mujibu wa ripoti.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amekuwa katika kiwango kizuri wiki za hivi karibuni, akipiga hat-trick dhidi ya Celtic katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Liverpool walipata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Bologna, shukrani kwa magoli ya Alexis Mac Allister na Mohamed Salah.

Raia huyo wa Misri ana mabao sita na asisti tano katika michuano yote lakini bado hajasaini mkataba wa nyongeza, huku mkataba wake wa sasa hapo Anfield unatarajiwa kumalizika msimu ujao wa joto.

Gazeti la Ujerumani, Bild linadai Wekundu hao wameanza kupanga mipango ya dharura iwapo Salah ataondoka na Adeyemi ni mmoja wa mlengwa wao.

Liverpool wanasemekana kutuma maskauti kumtazama mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani katika Bundesliga na wameeleza ada ya uhamisho ya euro milioni 50 ambapo wako tayari kulipa.




# Suárez amjia juu kocha wa Uruguay



**MIAMI, Marekani**

LUIS Suárez alifichua kile alichokiita mazingira magumu ya kazi yaliyowekwa na Kocha Mkuu wa Uruguay, Marcelo Bielsa, wakati wa Copa América 2024, kabla ya kuwataka mashabiki wasilaumu wachezaji ikiwa "kitu kitaenda vibaya".

Bielsa alijiunga na La Celeste Mei 15, mwaka jana na kuathiri mara moja jinsi timu ya taifa inavyofanya kazi, kwa mujibu wa Suárez.

"Wafanyakazi hawaruhusiwi kuingia na kutusalimia na kula nasi," alisema kwenye kipindi cha DirecTV .

"Lazima wawe waangalifu hata mlangoni waingie, inanipasua moyo kuwa hivi ndivyo maisha yalivyo kwenye viwanja leo... Matias Vecino ndiye aliyekuwa wa kwanza kuiona ikija.

Suárez aliendelea kutoa ufahamu juu ya athari za uongozi wa Bielsa wakati wa Copa América 2024, akielezea kukosekana kwa mawasiliano kati ya wafanyakazi wa benchi la ufundi na wachezaji.

"Kulikuwa na hali katika Copa América ambazo ziliniumiza, lakini sikusema kwa ajili ya kuishi pamoja," Suarez alisema kwenye kipindi hicho.

"Wachezaji wengi walifanya mkutano kumwomba kocha angalau atuage asubuhi, lakini hata hakutusalimia."

La Celeste walipata mkimbio mzuri kwenye Copa América 2024, na kumaliza katika nafasi ya tatu baada ya kuilaza Canada 2-2 (4-3) katika mikwaju ya penalti. Lakini zaidi ya matokeo, Suárez alionyesha picha mbaya nyuma ya pazia.

Fowadi huyo amestaafu kucheza timu ya taifa, akicheza mechi yake ya mwisho Septemba 6, mwaka huu. Aliondoka kama mfungaji bora wa muda wote wa Uruguay akiwa na mabao 69 katika michezo 143 katika kipindi cha miaka 17.

Bado, kabla ya kutundika jezi yake, Suárez alibainisha alizungumza na Bielsa kwa matumaini ya kuboresha hali ya sasa.

"Nilikuwa na mazungumzo ya dakika tano na Bielsa, nikizungumza kama kiongozi wa kikundi, na mwisho alijibu tu, 'Asante sana'," Suarez alisema.

HABARI MICHEZO

# FEI TOTO ANG'ARA, ATAMBA HESHIMA AZAM FC ITAREJEA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum ,Fei Toto' amefikisha pasi nne za mabao katika michezo ya Ligi Kuu Bara na kuisaidia timu yake kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Namungo, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi hapo juzi.

Fei Toto alipiga kona dakika ya 76 ambayo ilitua kichwani kwa Lusajo Mwaikenda na kuipatia Azam FC bao pekee kwenye mechi hiyo ya raundi ya saba.

Baada ya mechi kumalizika, Fei Toto aliwaambia mashabiki wa Azam kuwa na subira, akiahidi watarejea katika ubora uliozoeleka.

Kiungo huyo alisema wanaendelea kuimarika na wanatakiwa kuwa wavumilivu kwa sababu bado mwalimu wao ni mgeni, na amekuwa akifanya kazi kubwa.

"Mchezo ulikuwa mgumu kwetu, tumekosa ushindi michezo miwili iliyopita, mmoja tumefungwa na mmoja tukatoka sare, unajua mwalimu ni mpya, tunaendelea kufuata maelekezo yake kidogo kidogo, na waambia mashabiki wa Azam wasikate tamaa timu itakaa sawa," Fei Toto alisema.

Aliongeza si lazima yeye kufunga kama anaona hayupo kwenye eneo sahihi la kufanya hivyo, badala yake anachoangalia ni kuisaidia timu yake.

"Sijafunga bao lolote mpaka sasa, lakini ujue kufunga bao huwa inatokea kama unakaa sehemu sahihi, siyo unajiamulia tu, kama uko eneo la kutoa pasi basi inabidi utoe siyo kulazimisha kufunga, kwanza tunaangalia timu," alisema nyota huyo.

Ushindi huo unaifanya Azam kufikisha pointi 12 kwa michezo saba iliyocheza, ikishinda mechi tatu, sare tatu na kupoteza moja, ikiwa kwenye nafasi ya tano. Ulikuwa ni ushindi wa kwanza kwa Azam baada ya michezo miwili, ilipopoteza kwa mabao 2-0 dhidi ya Simba na Jumapili iliyopita ililazimishwa suluhu ugenini dhidi ya Mashujaa FC.

Kiungo huyo wa zamani wa Yanga, aliyemaliza Ligi Kuu msimu uliopita akiwa na ,asisti' saba, hajafunga bao lolote mpaka sasa, hata hivyo msimu uliomalizika alimaliza katika nafasi ya pili akiwa na magoli 19, akipitwa mabao mawili tu na mshindi wa kiatu cha dhahabu, Stephane Aziz Ki wa Yanga.

Baada ya kupoteza, Namungo inasalia na pointi zake sita, ikiwa imecheza michezo sita, nafasi yake ikiwa ya 12 kwenye msimamo wa Ligi Kuu.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Vijana ya umri chini ya miaka 20 (Ngorongoro Heroes), wakifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-20), yanayotarajiwa kufanyika kuanzia kesho jijini Dar es Salaam. **PICHA: TFF**

# TWFA kupata katibu mpya leo

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Utendaji ya Chama cha Mpira wa Miguu cha Wanawake Tanzania (TWFA), inatarajia kukutana leo ili kufanya uteuzi wa Katibu Mkuu mpya wa chama hicho, imeelezwa, jijini Dar es Salaam jana.

Nafasi ya Katibu Mkuu wa TWFA ilikuwa inashikiliwa na Somoe Ng'itu, ambaye kwa sasa ni Mwenyekiti mpya wa chama hicho baada ya kumshinda Amina Karuma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Somoe, alisema maandalizi ya kikao hicho yamekamilika na uteuzi huo unafanyika kwa mujibu wa matakwa ya katiba ya TWFA.

"Kikao kitafanyika kesho (leo), na hili linatekelezwa kwa kufuata katiba ambayo inaelekeza Makamu Mwenyekiti anateuliwa lakini anapata baraka za wajumbe wa mkutano mkuu wa TWFA kama ambavyo ilifanyika kule mkoani Kilimanjaro.

Kesho (leo), tunakwenda kufanya uteuzi ambao baraka zake zinatolewa na Kamati ya Utendaji, ninaamini wajumbe watatimiza majukumu yao katika kulikamilisha jambo hili," Somoe alisema.

Katika uchaguzi mkuu wa TWFA uliofanyika Septemba 14, mwaka huu, nafasi ya Makamu Mwenyekiti ilikwenda kwa Beatrice Mgaya kutoka Tanga, Zena Chande wa Dar es Salaam alifanikiwa kutetea nafasi yake ya Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa TFF.

Waliochaguliwa kuwa wajumbe wa Kamati ya Utendaji ni pamoja na Ndinagwe Sungura wa Rukwa, Irene Ishengoma (Dar es Salaam) na Hamisa Katambi kutoka mkoani Shinyanga.

# Uhamiaji yautaka ubingwa Zanzibar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

KOCHA Msaidizi wa Uhamiaji FC, Abdul-Salehe Abdallah, amesema lengo lake kubwa ni kuhakikisha timu hiyo inakaa kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Zanzibar kwa muda mrefu.

Uhamiaji FC imefanikiwa kuwafunga wanajeshi wenzao Kipanga bao 1-0 katika mechi ya ligi hiyo inayodhaminiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), iliyochezwa juzi jioni.

Matokeo hayo yanawafanya Uhamiaji kukaa katika nafasi ya kwanza na kuwashusha Mafaande wa JKU baada ya kufikisha pointi 10.

JKU yenye pointi tisa inafuatia katika msimamo huo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Zanzibar katika mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili, Abdallah, alisema timu yake iko katika mapambano ya mbio za ubingwa, hivyo hayuko tayari kupoteza nafasi yoyote watakayoipata katika kila mechi wanayocheza.

Kocha huyo alisema malengo yake ni kupata mafanikio na kila mechi watakayocheza kwao ni sawa na fainali.

"Tangu tumeanza ligi, huu ni mchezo wetu wa tano, bado mchuano ni mkali kwa kila timu ambayo inashuka uwanjani, hatutabweteka, tutaendelea kupambana hadi tutakapofikia malengo yetu," Abdallah alisema.

Aliongeza ingawa kwa sasa wapo kileleni katika msimamo wa ligi hiyo, anafahamu pointi walizonazo hazitoshi kuwafanya wakae hapo milele.

„Dhamira yetu ni kushinda michezo mingi zaidi kati ya michezo yetu 10 iliyobakia katika mzunguko huu wa kwanza. Tunahitaji kutimiza malengo ya kukaa kileleni kwa muda mrefu sio kwa muda mfupi, ingawa ligi ni ngumu sana hata utofauti wa alama unaonekana," alisema kocha huyo.

Alisema anaendelea kufanyia kazi mapungufu ndani ya kikosi chake ili kuhakikisha wanakuwa imara kuelekea mchezo unaofuata.

Michezo
Jumamosi Oktoba 5, 2024
Nipashe

Ten Hag: Wachezaji wangu 'walizimika'
UKURASA 21



# SIMBA YAVUTWA SHARUBU NYUMBANI

## ●●●Coastal Union yaipunguza kasi huku Camara akiokota...

**Na Adam Fungamwango**

IKITOKA nyuma, Coastal Union ilifanikiwa kurudisha mabao yote mawili iliyoruhusu kipindi cha kwanza na kulazimisha sare ya mabao 2-2 dhidi ya Simba katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana.

Wafungaji wa mabao hayo, Hassan Abdallah na Ernest Malonga, walikuwa wamemsoma kipa wa Simba, Moussa Camara, mwenye tabia ya kuacha lango lake mbali na kupachika mabao mepesi katika mechi hiyo na kugawana pointi.

Wakiwa nyuma kwa mabao 2-0, Hassan, aliupata mpira akiwa nje ya eneo la hatari, akapiga mpira wa juu uliokwenda moja kwa moja wavuni na kumwacha Camara asijue la kufanya.

Dakika ya 71, Malonga naye alifunga bao la pili baada ya Coastal Union kufanya shambulio la kushtukiza, kwa mguu wa kushoto alipiga juu, ukampita Camara na kujaa wavuni.

Baada ya mabao hayo, ndipo wachezaji wa Simba walionekana kushtuka wapo kwenye mechi na si mazoezi kama walivyokuwa wakifanya awali.

Haikucheza kwa kasi wala kiwango kilichozoeleka, wachezaji wakipiga pasi nyingi bila sababu yoyote, hawakutengeneza nafasi kama ilivyo kawaida, ikionekana kabisa waliingia wakidhani wanacheza na timu dhaifu.

Kipindi cha kwanza ilipata nafasi nyingi za kufunga, lakini wachezaji wake hawakuwa makini kuzitumia.

Ni sare ya kwanza kwa Simba baada ya michezo minne ya ushindi, huku Camara akiruhusu nyavu zake kutikiswa pia kwa mara ya kwanza.

Sare hiyo inaifanya Simba kupanda hadi nafasi ya pili na ikifikisha pointi 13 huku ikiishusha Fountain Gate iliyokuwa kwenye nafasi hiyo kutokana na kuwa na uwiano mzuri wa mabao ya kufunga na kufungwa. Pamoja na sare hiyo, bado Coastal Union inasalia nafasi ya 13 licha ya kufikisha pointi tano, imepata sare ya pili katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mechi ilianza taratibu kila timu ikionekana kusoma mchezo wa mwenzake, na ikicheza kwa dakika 15 bila ya kila upande kufanya shaambulizi lolote la maana langoni.

Coastal Union ilikuwa na mpango mkakati wa kukaa nyuma ya kuwaachia Simba mpira ambao walikuwa wakifanya kazi ya kuifungua ngome ya Wagosi wa Kaya.

Baada ya magolikipa wote kuwa likizo, hatimaye dakika ya 15, Jean Charles Ahoua, alimwamsha, Matampi, baada ya shuti lake kutoka nje kidogo ya lango.

Alimegewa pande nje kidogo ya eneo la hatari na Debora Fernandes, kabla ya kupiga shuti hilo lililomshughulisha kipa huyo kwa kuruka, lakini mpira ulitoka nje ya lango.

Simba ilifanikiwa kuandika bao la kwanza dakika ya 25 baada ya kufanya shambulizi ambalo hakuna aliyetarajia kuwa lingezaa bao.

Beki wa kulia, Shomari Kapombe, alitoka na mpira kwenye wingi ya kulia akiwa amepewa pasi na Joshua Mutale, akaupiga ndani ya lango ukamkuta tena winga huyo wa Mzambia ambaye aliupiga mpira wa juu, Matampi aliruka juu na kuudaka, lakini alipofika chini ulimponyoka mbele ya Leonel Ateba na Mohamed Hussein ,Zimbwe Jr', ambaye aliukwamisha wavuni na kuandika bao la kwanza katika mchezo huo.

Pamoja na kufunga bao hilo, Coastal Union bado hawakushawishika kuondoka langoni mwao, badala yake waliendelea kujaza wachezaji wengi, lakini wakishambulia kwa kushtukiza, mashambulizi ambayo hayakuwa na hatari sana kwa wapinzani wao.

Dakika 14 baadaye, straika raia wa Cameroon, Ateba alifunga bao lake la pili msimu huu, pia kwenye mchezo huo kwa penalti baada ya beki, Abdallah Denis ,Viva', kuunawa ndani ya eneo la hatari kutokana na harakati za kuokoa hatari hiyo.

Mabadiliko ya timu zote ya kipindi cha pili yaliisaidia zaidi Coastal Union badala ya Simba.



Kipa wa Coastal Union, Levy Matamp (kushoto), akiwahi kudaka mpira dhidi ya beki wa kati wa Simba, Abdulrazak Hamza (aliyeruka juu), katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam jana. Timu hizo zilitoka sare ya mabao 2-2. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## Gamondi: Mipira ya faulo 'kuwaua'

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Miguel Gamondi, amezitahadharisha timu za Ligi Kuu Tanzania Bara zitapata 'tabu' kuwazuia wachezaji wake kufunga mabao kwa kutumia mipira ya faulo kwa sababu tayari mafunzo anayowapatia yameshaanza kufanya kazi.

Gamondi amesema amegundua katika Ligi Kuu Tanzania Bara, mipira ya faulo inapatikana mingi, lakini imekuwa haitumiwi vizuri, hivyo ametengeneza mafunzo maalum kwa nyota wake ili waweze kupata mabao kwa njia hiyo.

Kocha huyo alisema hayo baada ya mechi dhidi ya Pamba Jiji iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam na timu yake kuondoka na ushindi wa mabao 4-0. Beki wa kati, Ibrahim Hamad ,Bacca', kwa mara nyingine tena alifunga bao akiunganisha kwa kichwa mpira wa faulo iliyopigwa na Maxi Nzengeli. Licha ya kuwa ni bao la pili kwa Bacca, pia ni la pili lililotokana na mpira wa faulo, kama ilivyotokea, Septemba 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine, Mbeya dhidi ya KenGold, alipopachika bao kwa kichwa, kutokana na faulo iliyopigwa na Stephane Aziz Ki na kuwa bao pekee katika mchezo huo.

„Kwa sasa tumejifunza jinsi ya kupata mabao kwa njia ya faulo, kila kitu tumekifanyia mazoezi, katika ligi ya Tanzania wachezaji wanafanya faulo nyingi sana, kama zinatumiwa vizuri, tunaweza kupata mabao mengi na ndivyo ninavyofanya sasa," alisema Gamondi.

Kocha huyo alifurahishwa pia na safu yake ya ulinzi kuwa imara kwa kucheza michezo nane bila kuruhusu nyavu zao kutikiswa.

"Ikumbukwe tuna rekodi safi ya kucheza michezo nane bila kuruhusu bao, mara ya mwisho ilikuwa ni kwenye fainali ya Kombe la FA dhidi ya Azam FC, hii ni kazi kubwa ya mabeki wangu, wakisaidiwa na wenzao," alisema kocha huyo raia wa Argentina.

Aliongeza alijua Pamba Jiji wangeingia na staili ya kupaki basi, hivyo akawaandaa wachezaji wake kucheza na timu ya aina hiyo.

Ushindi huo umewafanya Yanga kufikisha pointi 12, ikishika nafasi ya nne katika msimamo wa ligi hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >